

**KUCHUNGUZA MAUDHUI YA NYIMBO ZA KAMPENI ZA UCHAGUZI
MKUU ZANZIBAR 2000-2010**

DAUD MOH'D ALI

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2017

UTHIBITISHI

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu yenye mada: **“Kuchunguza Maudhui ya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu Zanzibar 2000-2010”** na kupendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Prof. Dkt. Sheikh.T.S.Y.M.Sengo

(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

IKIRARI

Mimi, **Daud Moh'd Ali**, ninathibitisha kwamba, tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote, kwa ajili ya kutunukiwa Digrii yoyote.

.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa watu muhimu kwangu, kwanza, wazazi wangu wapendwa marehemu baba yangu bwana Moh'd Ali Shamata na mama yangu bibi Mkasi Khamis Khatib (Mungu awalaze mahali pema peponi, amin), ambao kwa pamoja wamejitolea kwa hali na mali kufanikisha matarajio yangu ya kielimu yaliyoniwezesha kufikia hatua hii. Pili, mke wangu mpenzi Zakia Iddi Ali, watoto wangu wapendwa, dada, ndugu na kaka zangu wote wa ukoo wa Shamata Mustafa, kwa pamoja ninawatunukia zawadi hii adhimu kwao.

SHUKURANI

Awali ya yote ninapenda nimshukuru Mwenteezi Mungu, Muumba mbingu na ardhi kwa kunijaalia nguvu, uhai, uzima, uwezo na jitihada kukamilisha utafiti huu. Utafiti huu umekamilika kutokana na msaada wa watu tafauti. Si rahisi kuwataja wote. Hata hivyo, nitawatataja baadhi kwa niaba yao. Kwanza ninamshukuru kwa dhati msimamizi wangu Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M Sengo kwa kuniongoza katika kukamilisha kazi hii. Pili, ninawashukuru wazazi wangu wapendwa kwa kujitolea kwa hali na mali kunipeleka skuli na kunisimamia hadi kupata akili zilizoniwezesha kufikia kiwango cha uzamili huu.

Tatu, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa mke wangu mpendwa Zakia Iddi Ali, kwa ustahamilivu na ushirikiano wake kwa kipindi chote cha masomo yangu. Nne, mwalimu Mmanga Mjengo Mjawiri wa Chuo Kikuu Cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ushirikiano wake hadi nikapata data zilizokamilisha utafiti huu. Ninamshukuru kaka yangu Issa Khamis Issa kwa kunikutanisha na wana kikundi cha sanaa, mila na utamaduni cha Zanzibar. Pia wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kushirikiana nami katika harakati za masomo.

Shukrani za pekee zimwendee Dkt. Maulid Haji Omar, kwa kunipa maelekezo na msaada wa kutosha hadi kukamilika kwa utafiti huu. Walimu na wanafunzi wote wa Chuo Kikuu cha Suza. Baraza la Sanaa na Muziki Zanzibar. Mwisho, viongozi wote wa vikundi vya Ngoma na Taarab, kwa kushirikiana nami hadi kukamilika kwa utafiti huu.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar (2000-2010). Mtafiti aliongozwa na madhumuni mahsusi matatu, la kwanza, kuchunguza na kuainisha nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar 2000-2010, la pili, Kutathmini mchango wa nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar, katika kustawisha jamii ya Wazanzibari, na la tatu, Kutafuta mbinu za kufanya nyimbo hizo ziwe zinaleta umoja badala ya utengano katika jamii ya Wazanzibari. Katika kufanikisha madhumuni hayo, mtafiti alifuata njia zilizostahiki kwenda kwenye vikundi vya ngoma na kukutana na malenga ili kupata data alizozihitaji kwa watafitiwa. Watafitiwa hao waligawanyika katika makundi ya vijana, watu wazima wenye maarifa na kumbukumbu za mambo ya kihistoria, walimu, wasanii, wataalamu wa lugha ya Kiswahili na utamaduni, na waandishi wa habari. Mtafiti aliongozwa na nadharia ya mtu na Utamaduni, nadharia ya Fasihi ina kwao, nadharia ya Tabia na nadharia ya Uhalisia katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Aidha, utafiti umetaja kipengele cha lugha, wahusika na mandhari ili kuibulia maudhui yaliyokusudiwa. Utafiti umeonesha dhamira ya kuhamasisha, ajira kwa vijana, na mmomonyoko mkubwa wa maadili ya jamii. Mwisho, utafiti umetoa mapendekezo kwa watafiti wa usoni.

YALIYOMO

UTHIBITISHI	ii
HAKIMILIKI.....	iii
IKIRARI	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiii
ORODHA YA VIAMBATISHO.....	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Usuli wa Tatizo	3
1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti	8
1.5 Lengo la Utafiti	8
1.6 Madhumuni Maalumu	8
1.7 Maswali ya Utafiti	8
1.8 Umuhimu wa Utafiti.....	9
1.9 Mipaka ya Utafiti	10
1.10 Matatizo ya Utafiti na Utatuzi Wake.....	10
1.10.1 Kiutawala	10

1.10.2	Kuwapata Wahojiwa	11
1.10.3	Kuwapata Wasanii.....	11
1.10.4	Matatizo ya Kijamii.....	11
1.10.5	Matatizo ya Kitaalimu	11
1.11	Mpangilio wa Tasnifu	12
1.12	Hitimishi.....	12
SURA YA PILI.....		13
UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA		13
2.1	Utangulizi	13
2.2	Maana ya Fasihi Simulizi	13
2.3	Maana ya Nyimbo	14
2.4	Histori ya Nyimbo	16
2.5	Sifa za Nyimbo.....	19
2.6	Aina za Nyimbo	20
2.6.1	Nyimbo za Tumbuizo.....	20
2.6.2	Kongozi	21
2.6.3	Nyimbo za Uganga.....	21
2.6.4	Nyimbo za Dini	22
2.6.5	Wawe.....	23
2.6.6	Tenzi.....	23
2.6.7	Tendi.....	23
2.6.8	Mbolezi.....	23
2.6.9	Kimai	23
2.6.10	Nyiso	24

2.6.11	Nyimbo za Vita	24
2.6.12	Nyimbo za Kazi.....	25
2.6.13	Nyimbo za Uwindaji	25
2.6.14	Nyimbo za Watoto	25
2.6.15	Nyimbo za Taifa.....	27
2.6.16	Nyimbo za Siasa.....	27
2.7	Fani Katika Nyimbo	28
2.7.1	Utangulizi	28
2.7.2	Vipengele vya Fani.....	29
2.8	Mapitio ya Maandishi.....	31
2.9	Mkabala wa Nadharia.....	38
2.10	Maelezo ya Dhana Muhimu	38
2.10.1	Nadharia ya Mtu na Utamaduni	38
2.10.2	Nadharia ya Fasihi ina Kwao	39
2.10.3	Nadhariya ya Tabia	40
2.10.4	Nadharia ya Uhalisia	41
2.11	Hitimishi.....	44
	SURA YA TATU	45
	MBINU ZA UTAFITI.....	45
3.1	Utangulizi	45
3.2	Mkabala wa Utafiti.....	45
3.3	Eneo la Utafiti	45
3.4	Mbinu za Utafiti	46
3.4.1	Mbinu ya Maktabani	46

3.4.2	Mbinu ya Masikanini (Makaazini)	47
3.4.3	Mbinu ya Usaili	47
3.4.4	Mbinu ya Hojaji	48
3.4.5	Watafiti Wasaidizi	49
3.5	Uteuzi wa Watafitiwa	50
3.5.1	Vijana	51
3.5.2	Watu Wazima	51
3.5.3	Walimu	52
3.5.4	Wasanii	52
3.5.5	Wasomi	52
3.5.6	Wataalamu wa Lugha ya Kiswahili	53
3.5.7	Waandishi wa Habari	53
3.6	Ukusanyaji wa Data	54
3.7	Zana za Kukusanyia Data	54
3.8	Hitimishi	55
	SURA YA NNE	56
	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA	56
4.1	Utangulizi	56
4.2	Kukusanya na Kuainisha Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar 2000-2010	57
4.3	Kutathmini Michango ya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar Katika Kustawisha Jamii ya Wazanzibar	64
4.3.1	Kuburudisha	64
4.3.2	Kuhamasisha	65

4.3.3	Ajira kwa Vijana	67
4.3.4	Kujenga Maadili	67
4.4	Kutafuta Mbinu za Kufanya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Ziwe.....	
	Zinaleta Umoja Badala ya Utengano Katika Jamii ya Wazanzibari	68
4.5	Uchambuzi wa Maudhui ya Nyimbo za Kampeni	69
4.5.1	Umoja wa Jamii ya Wazanzibari.....	71
4.5.2	Maadili	72
4.5.3	Mila na Utamaduni.....	73
4.5.4	Migogoro	77
4.6	Hitimishi.....	80
	SURA YA TANO.....	81
	MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO	81
5.1	Utangulizi	81
5.2	Muhutajari wa Tasnifu.....	81
5.3	Matokeo ya Utafiti	82
5.4	Mapendekezo ya Utafiti	83
5.5	Mapendekezo Juu ya Utafiti Fuatishi.....	84
	MAREJELEO	85
	VIAMBATANISHI	90

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Namba 3.1: Jumla ya Watafitiwa 31 53

ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatanishi 1: Nyimbo za Kampeni	90
Kiambatanishi 2: Hojaji kwa Walimu na Wasomi.....	117
Kiambatanishi 3: Muongozo wa Mahojiano na Wadau Mbalimbali wa Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar Wakiwemo Wasanii, Vijana, Walimu, Wataalamu wa Lugha ya Kiswahili, Wasomi na Waandishi wa Habari	122

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amezungumzia kwa kina kuhusu chimbuko na tatizo la utafiti huu. Utafiti huu unahusu maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar: (2000-2010). Mtafiti amekusudia kubainisha usuli wa mada ya utafiti kwa kufafanua fasili za nyimbo na umuhimu wa nyimbo. Mtafiti amezungumzia usuli wa tatizo kwa kuonesha sababu za mivutano na uhasama uliyotokea wakati wa kampeni za chaguzi zilizopita Visiwani, na kuonesha mivutano, ubaguzi na uhasama unaozaga wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar. Utafiti huu umefanywa katika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

1.2 Usuli wa Mada

Historia ya Zanzibar ni pana na ni yakale sana. Historia ya Visiwa hivi imeanza miaka na karne nyingi zilizopita. Visiwa hivi ni sehemu ya kumbukumbu ya historia ya ulimwengu, Waajemi wafanyabiashara, walivigundua na kuvifanya makao makuu kwa safari kati ya Mashariki ya Kati, India na Afrika. Kabla ya wafanyabiashara hao kuingia Zanzibar, watu wa asili walikuwa ni wavuvi, wakulima na wafugaji. Mila na dasturi zao, ni za kupendana, kuishi pamoja, kufanyakazi zao pamoja kwa ujima uliodumisha mafahamiano ya pamoja. Watu hao wa Zanzibar, walikuwa na tawala zao za jadi.

Sheriff (1995) anasema, utawala wa jadi wa watu wa Zanzibar ulikuwa ni wa wakuu wa vijiji. Kila kijiji kilikuwa kikiongozwa na mtu ambaye aliheshimiwa

kutokana na kuhamia eneo hilokabla ya wengine na kuonekana kuwa ni muasisi wa kijiji. Kiongozi huyo ndiye aliyekuwa na uwezo kamili wa kuamua na kuagiza. Pamoja na uwezo alionao kiongozi huyo, alikuwa akiteuwa wasaidizi wake kutoka katika koo mbalimbali ili maoni na fikra zao ziweze kusaidia kufikia uamuzi wa busara na wa pamoja. Viongozi hao wateuliwa walikuwa na maarifa ya mambo mengi yaliyohusu jamii zao na yaliyoaminika mbele ya wenzao, waliunda Baraza la wazee ambalo ndilo lililokuwa na kauli ya mwisho kuhusu mambo yote ya kijijini hapo na watu wote walikuwa wakifuata maelekezo na ushauri uliotolewa na baraza hilo kwa pamoja.

Utawala huo ulirithiwa na kizazi cha muasisi huyo. Watu hao walikuwa na dasturi zao za jadi, katika kufanya sherehe na mambo yao ya kijamii. Nyimbo zilitumika sana katika shughuli zao nyingi za kijamii, kama vile sherehe, ikiwemo hatua anayopitia mwanajamii yeyote, yaani kuzawa, kupewa jina, jando, unyago na harusi. Pia nyimbo zilitumika katika sherehe zilizohusu mambo ya kila siku kama vilekazi, michezo na anapotawazwa kiongozi mpya.

Zanzibar, (2014) anasema, mnamo miaka ya 1870, wakati Zanzibar ikitawaliwa na Mfalme Sayyid Said Bin Baraghash, nyimbo zilitumika sana kuwaburudisha na kuwaliwaza Mfalme na aila yake kwenye kumbi zilizokuwemo kweye makasri yao. Machano (2015), alipokuwa akizungumza na mtafiti, alisema, nyimbo hizo, ziliimbwa kwa lugha ya Kiarabu kwa sababu, hao watawala walikuwa ni Waarabu. Nyimbo hizo ziliendelea kuimbwa kwa Kiarabu, kuwasifu mabwana na ufalme wao, hadi wakati wa utawala wa Sultani Baraghashbin Said, ambaye alianzisha matumizi

rasmi ya Lugha ya Kiswahili. Akiendelea, Machano alisema, hadhi ya nyimbo hizo zilibadilika kutoka kwa walio na hadhi na wa tabaka la juu na kuwa za kina yakhe. Mabadiliko haya yalitokana na mfumo wa jamii kubadilika, jamii ilipoanza kudai uhuru wa kujitawala.

Nasser (1999) anasema, mpaka katika miaka ya 1960, Zanzibar, iliongoza kwa kila Jambo kama vile, uchumi mzuri, ustaarabu na maendeleo, katika Afrika Mashariki na kwengineko. Katika miaka ya 1930 kulitokea mzozo wa nauli za usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka shamba na kuja mjini, mzozo huo ulitokana kwa kupandishwa bei ya nauli. Hapo kulianzishwa chama cha Muawana kilichoitwa Ittihad Al- Watan Chama Cha Umoja wa Wananchi. Madhumuni yake ilikuwa ni kumiliki mabasi ili wananchi wa mashamba waweze kupata nafuu ya nauli. Nasser aliendelea, Chama hicho, baada ya kufanya huduma zake hizo, kilileta hisia za umoja wa udugu, mawasiliano, masikilizano na mafahamiano mema baina ya watu wa shamba na watu wa mjini. Jambo hilo lilisaidia sana kuundwa kwa chama cha mwanzo cha siasa Zanzibar, Zanzibar Nationalist Party (Z N P) mnamo miaka ya 1950 na kuwa mwanzo wa harakati za kuundwa vyama vingi vya siasa Zanzibar, kikiwamo Afro-Shirazi Party (A S P) mwaka 1957 na Zanzibar and Pemba People's Party (Z P P P) mwaka 1959. Nyimbo zilitumika kuhamasisha, kuunganisha na kujenga umoja miongoni mwa wanachama wa vyama hivyo. Pia, nyimbo zilitumika kuvisema vyama vyengine.

1.3 Usuli wa Tatizo

Jamii ya Wazanzibari ni ya mchanganyiko wa watu. Ni watu waliochanganya rangi na damu za makabila mengi kutokana na historia ya maumbile ya visiwani. Watu hao

waliishi kwa maisha ya udugu wa asili; kukaa pamoja, kusaidiana kwa kila hali na mali kwa miaka mingi. Nasser (1999) anasema, Kwa mtazamo wa Nasser, Zanzibar ina wenyewe, na wenyewe hao ni watu wenye asili tafauti, wakiwamo; Waafrika wa Mrima na wa Mwambao wa Afrika Mashariki, watu hao wa karibu na wa mbali ambao walikuja kwa haja zao.

Watu hao waliishi kwa ushirikiano mkubwa kwa karne nyingi zilizopita. Sheriff, (1991) anasema, mnamo karne ya kumi na tisa (19), Zanzibar ilitawia kiuchumi na ilikuwa ni Taifa lenye utajiri mkubwa katika eneo lote la mwambao wa Bahari ya hindi na kufikia kuwa nchi tajiri kuliko zote Afrika. Utajiri wa Zanzibar, wakati huo, ulitawia sana na ustaarabu wa watu wa Zanzibar uliwavutia watu wa mataifa mengi. Kila mtu aliyepata habari ya Zanzibar wakati huo alitamani kufika ili ajionee mwenyewe, ndipo kukawapo msemu, “Zanzibar ni njema atakae na aje”.

Sheriff, (1991) anasema, Waingereza waliingia Zanzibar mnamo mwaka (1897) kwa kisingizio cha kusafisha biashara ya utumwa. Walipofika, walianza kuwapa elimu wenyeji iliyokuwa inakasumba ya ubaguzi. Waliwajaza chuki za kitumwa zilizosababisha ukabila miongoni mwa Wazanzibari. Chuki hizo za utumwa, ukabila na udini zilanzishwa kwa kusingizia Waarabu na Waislamuati ati ndio walianzisha na walioendeleza biashara ya utumwa hali ya kuwa biashara hiyo iliendeshwa na Wazungu wenyewe.

Nasser (1999), ameeleza sababu za ufisidi na mivutano, zilianza Wazungu walipofika Zanzibar na kutaka kuchukuwa utajiri uliyokuwepo kwa maslahi yao na ya nchi zao. Umoja wa Wazanzibari na ustawi wao ulizidi kuvunjika pale Waingereza

walipostawisha utawala wao na kuwagawa wananchi kwa hadhi na makabila ili kufanikisha utawala wao kwa kutumia mbinu ya wagawe, tuwatawale.

Mapuri (1996) ameeleza kuwa, baada ya biashara ya utumwa kuwashinda Wazungu hao kuiendesha, Waingereza waliigawa jamii ya Wazanzibari katika daraja tano, daraja ya kwanza, Wazungu, ambao walikuwa na mamlaka makubwa. Daraja ya pili, Waarabu, waliokuwa wanamiliki mali, daraja ya tatu, Wahindi, ambao walikuwa wafanya biashara, daraja ya nne, walikuwa Machotara na Wangazija. ambao walitumiwa kama makarani na chombo cha starehe, na kundi la tano, lilikuwa ni la Waafrika Waswahili weusi. Kwa mtazamo wa Mapuri mgawanyiko huo ndicho kitendawili na ndiyo ndwele iliyotusibu hadi leo. Mbogo (2015) anasema wakoloni, Waingereza, kabla ya kuondoka Visiwani walimkabidhi Sultani Jamshid Uhuru na mamlaka ya kuitawala Zanzibar tarehe 1/12/1963. Wazanzibari waliowengi na hasa Waafrika weusi, waliona kuwa ule ulikuwa ni Uhuru wa bandia uliokuwa na lengo la kuendeleza usultani, Umwinyi na Ukandamizaji. Pamoja na yote hayo, Mapuri alieleza siasa za chuki zilizoanzishwa na Waingereza mwaka (1957), kufanyika chaguzi tafauti kama vile, uchaguzi wa 1957, 1961, 1963. Uchaguzi wa mwaka 1957 ulikuwa ni wa kwanza kufanyika. Katika uchaguzi huo, watu sita (6) walisimama kupigania kuingia katika Baraza la kutunga sharia. Majimbo manne yalikuwa Unguja na mawili Pemba. Matokeo ya uchaguzi huo, Chama Cha A S P kilipata viti vitatu (3) Unguja, Z N P hakikupata hata kiti kimoja. Kiti kimoja cha mjini Unguja alikipata bwana Chodhry, mwakilishi wa Chama cha Waislamu, na vile viti viwili vya Pemba kimoja alikipata bwana Muhammad Shamte na cha pili, Bwana Ali Shariff wote hao walisimama binafsi.

Uchaguzi wa pili ulikuwa wa Juni 1961. Katika uchaguzi huo viti ishirini na mbili (22) viligombaniwa. Matokeo;

A S P	viti	10
Z N P	viti	09
ZPPP	viti	03
Jumla	viti	22

Katika matokeo hayo hakukuwa na chama kilichoweza kuunda serekali peke yake bila kushirikiana na chama kingine. Kutokana na hali hiyo, ilibidi kuitishwa uchaguzi mwengine baada ya miezi sita.

Uchaguzi wa marejeo ukawa ni wa tatu. Ukafanyika tarehe 1 Juni 1961, ukiwa wa kugombea viti 23 badala ya 22 kuepusha kutokea idadi sawa ya viti. Katika uchaguzi huo ZPPP walishirikiana na Z N P na matokeo ya uchaguzi huo yakawa;

ZPPP na ZNP	viti	13
A S P	viti	10
Jumla	viti	23

Matokeo ya uchaguzi huo yalichochea na Wazungu waliokuwapo wakati huo na kuzuka mapambano yaliyopelekea vita vya Juni baina ya wafuasi wa A S P na ZPPP na ZNP.

Mwaka 1963 Mwezi wa Julai, ulifanyika uchaguzi wa nne. Uchaguzi huo ulikuwa wa kuchagua wajumbe 31 wa Baraza la Taifa (National Assembly). Kupelekea uhuru wa Zanzibar. Matokeo yalikuwa:

Z N P na Z P P P	wajumbe	18
A S P	wajumbe	13
Jumla	wajumbe	31

Kutokana na matokeo hayo ZNP na ZPPP waliunda Serikali chini ya mamlaka ya Waingereza. Baada ya hapo viongozi wote wa vyama vya siasa walitakiwa waende London kwa mazungumzo ya Katiba na Uhuru. Huko London viongozi wote walikubaliana Zanzibar ikabidhiwe uhuru wake Disemba 1963. Makubaliano hayo yalitekelezwa. Uhuru wa Zanzibar ulitolewa Disemba 1963, chini ya usimamizi wa Uingereza lakini viongozi wa AS P hawakuridhika, tarehe 12 Januari 1964 wakafanya mapinduzi kupindua Serikali ya ZNP na ZPPP. Mapinduzi hayo hadi leo hayakuwafurahisha wafuasi wa ZNP Na ZPPP.

Pamoja na siasa ya Mapinduzi ya 1964 iliyochangia kwa kiasi kikubwa, mivutano na uhasama. Vile vile, mfumo wa vyama vingi ulipoanzishwa tena mwaka 1992, ulichukuliwa na ulipokelewa kwa mtazamo wa kihistoria. Uzushi wenye kuzidisha chuki, umekuwa ukitapakazwa na kutiwa chumvi ya kila namna ili kuzidisha sumu za ukabila na udini miongoni mwa Wazanzibari na majirani zake. Nyimbo zilitumika kama nyenzo ya kuhamasisha jamii katika shughuli hizo, Mapuri (1996).

Pengo la kutokuwapo kwa ripoti ya utafiti wa maudhui ya nyimbo za kampeni kwa kipindi chote hicho, na tatizo la mivutano na uhasama inayotokea wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar ni kitendawili. Jamii ya Wazanzibari haijuwi maudhui ya nyimbo hizo. Hali hii iliongeza chachu katika tatizo na ndiyo iliyomtiya shauku mtafiti kufanya utafiti huu.

1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Mivutano, uhasama na ubaguzi unaozagaa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu Zanzibar, ni tishio kwa wanajamii wote wa Visiwani Zanzibar. Hali hii imezusha tatizo la nyimbo zinavyotumika katika kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar. Ni tatizo kubwa lisilopuuzika na lililohitaji kutafutiwa utatuji. Hayo ndiyo yaliyomfanya mtafiti kutaka kuchunguza kwa vipi na kwa nini nyimbo zilitumika katika kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar?

1.5 Lengo la Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza na kuchambua maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu wa Zanzibar, kuanzia mwaka 2000 hadi 2010, katika kustawisha jamii ya watu wa Zanzibar.

1.6 Madhumuni Maalumu

Utafiti huu una madhumuni yafuatayo;

- (i) Kukusanya na kuainisha nyimbo za kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar 2000-2010.
- (ii) Kutathmini mchango wa nyimbo za kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar katika kusitawisha jamii ya Wazanzibari.
- (iii) Kutafuta mbinu za kuzifanya nyimbo za kampeni za uchaguzi zilete umoja badala ya utengano katika jamii ya Wazanzibari.

1.7 Maswali ya Utafiti

- (i) Ni nyimbo gani, hutumika katika kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar?

- (ii) Jee nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar zina mchango gani katika kustawisha jamii ya Wazanzibari?
- (iii) Ni mbinu zipi zinazoweza kutumika ili nyimbo za Kampeni za Uchaguzi, Mkuu wa Zanzibar zisaidie kuimarisha chaguzi hizo ili kuleta umoja kwa Wazanzibari badala ya utengano?

1.8 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ukikamilika utakuwa na umuhimu mkubwa kwa jamii ya Wazanzibari.

Kisanaa: Wasanii watapata msingi imara ili kuweza kutunga na kuimba nyimbo za kuhimiza umoja na maelewano ndani ya jamii ya Wazanzibari, jambo ambalo litasaidia kuimarisha umoja na maelewano miongoni mwa wanajamii badala ya kuleta mifarakano wakati wa kampeni za uchaguzi.

Kisiasa: Wanasiasa watanufaika katika kampeni zao, kwani wataelewa kwa kiasi gani wanaweza kuzitumia nyimbo kuwafikishia ujumbe wanajamii na kuwatimizia makusudio yao. Aidha, utafiti huu utawafanya wanasiasa kujua mipaka yao, ili waweze kuzitumia nyimbo ndani ya kampeni za uchaguzi bila kuleta athari hasi. Tajriba kama hizo zitaleta ustahamilivu wa kisiasa na kijamii na kuwezesha jamii kuishi kwa amani na utulivu. Ni matarajio yetu kwamba, jamii itafahamu maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi na kujijua ipo wapi, inatoka wapi, na inapelekwa wapi.

Kitaalimu: Matokeo ya utafiti huu yatakuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taalimu ya fasihi. Wanafunzi watakaoyatumia matokeo ya utafiti huu watayafanya kuwa sehemu ya madondoo yao ya kukamilishia maudhui ya utafiti wao

watakaokuwa wameufanya. Kwa walimu wa Skuli za Sekondari, watayatumia matokeo ya utafiti huu kuwafundishia wanafunzi wao mada ya uchambuzi na uhakiki katika fasihi simulizi madarasani mwao.

1.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umechambua maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar 2000-2010 tu. Uchambuzi uliyofanywa katika utafiti huu ni wa kifasihi ambao uliongozwa na nadharia teule za uhakiki wa kifasihi. Kwa upande wa mipaka ya Kimaeneo, utafiti huu, umefanyika Zanzibar, katika kisiwa cha Unguja, Mkoa wa Mjini Magharibi, wilaya ya Mjini. Eneo hili limechaguliwa kwa sababu ni sehemu inayokusanya watu kutoka sehemu zote za Visiwani na ni sehemu inayoanzia mambo yote. Unguja Mjini ndipo kitovu na kituo cha mambo yote muhimu ya maisha na uendeshaji wa Utawala wa Serikali. Kwa hivyo ni rahisi kupatikana data zilizohitajika kwa wepesi na kwa hakika.

1.10 Matatizo ya Utafiti na Utatuzi Wake

Katika kufanya kazi hii kuna matatizo mengi yaliyomfika mtafiti. Miongoni mwa matatizo hayo ni:

1.10.1 Kiutawala

Mtafiti alipata matatizo mengi ya kiutawala, miongoni mwa hayo ni safari za kufuatilia utafiti huu, kununua vifaa vilivyosaidia utafiti, kama karatasi, kucharaza, kuchapa, kutowa vivuli n.k. Gharama ni tatizo lakini ‘Ukitaka uzuri, lazima udhurike’. Mtafiti alitumia akiba aliyojiwekea kuifanya kazi ya utafiti huu.

1.10.2 Kuwapata Wahojiwa

Nyimbo za kampeni zimehusisha vyama vya siasa vyenye mitazamo tafauti. Kuwapata wahojiwa haikuwa kazi nyepesi. Vile vile baada ya kuwapata, kukubali kutoa majibu sahihi, bado likabakia kuwa ni tatizo jingine. Mtafiti alitumia uzowefu wake wa uwalimu wa muda mrefu, hekima na busara kukutana na watu anao watambuwa, katika kila kundi ili kusaidia kuwapata wahojiwa wa rika zote waliosaidia kukamilisha kazi yake.

1.10.3 Kuwapata Wasanii

Wasanii wengi wamedhaminiwa na vyama vyao. Kumpata msanii, kisha akakubali kutoa nyimbo zake na maelezo ya nyimbo hizo, ilikuwa kazi iliyohitaji maarifa na ujasiri mkubwa, haikuwa kazi nyepesi. Asiyekujua hakuthamini; na waimbaji wengi wa nyimbo hizo za kampeni, huwa kwenye mapambano ya kisiasa, ni vigumu kama mtu hamjuwi kumpatia nyimbo zao. Mtafiti alitumia watu mashuhuri wa ndani ya vikundi vya ngoma, kupewa yaliyomo ndani ya siri zao.

1.10.4 Matatizo ya Kijamii

Mtafiti ni mwanajamii. Ndani ya jamii, kuna mambo mengi; kama vile: harusi, misiba, maradhi na mengine. Hayo yote yaliweza kuathiri kazi ya utafiti kwa wakati aliyokusudia mtafiti. Kwa kuwa 'shida huzaa maarifa' Mtafiti alijipanga vizuri kuyakabili yote yaliyotokea kwa utaratibu uliyomwezesha kukamilisha utafiti wake kwa wakati uliyopangwa.

1.10.5 Matatizo ya Kitaalimu

Matatizo ya upungufu wa vitabu katika maktaba zilizopo Zanzibar na vyanzo vyengine kama vile, tasnifu za watangulizi, Mtafiti alitafuta Maktaba zenye uhakika

wa kupata vitabu na tasnifu zilizoko Dar es Salam, ambako alifanikiwa kusoma vyanzo vyengine, kama majarida yaliyomsaidia kupata data za kukamilishia utafiti wake.

1.11 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura kuu tano, zenye mada ndogondogo ndani yake. Sura ya kwanza inaeleza vipengele vya kiutangulizi. Vipengele hivyo ni; usuli wa mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo la utafiti, madhumuni maalumu ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, matatizo ya utafiti na utatuzi wake na mpangilio wa utafiti. Sura ya pili inaeleza utalii wa kazi tangulizi. Sura ya tatu inawakilisha njia na mbimu za utafiti. Sura ya nne ni uchambuzi wa data za utafiti na sura ya tano ni muhtasari, hitimishi na mapendekezo ya utafiti.

1.12 Hitimishi

Sura hii ya kwanza imefafanua mada ya utafiti kwa kutoa utangulizi, usuli wa mada, kutoa maelezo kuhusu chanzo cha tatizo la utafiti na kulitaja tatizo la utafiti. Pia lengo la utafiti, madhumuni na maswali ya utafiti. Umuhimu na matatizo ya utafiti, vyote hivyo vimefafanuliwa katika sura hii. Sura inayofuata inahusu utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia.

SURA YA PILI

UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, kazi za watangulizi zilisomwa kwa makini, maelezo juu ya nyimbo na burudani yamejadiliwa. Utafiti una siri, na usilolijua ni usiku wa kiza; ”Siri ya mtungi kaiulize kata” na ”utamu wa ngoma, uingie uicheze” Mtafiti amekusudia kutalii vyanzo vya vitabu, makala, tasnifu, masimulizi ya mdomo pamoja na wavupepe, ili kupata mawazo yaliyotangulia pamoja na maalumati yanayohusu Nyimbo, na hasa Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi. Mwanzo kabisa, alivisoma vitabu, vilivyotowa muongozo wa ufanyaji wa utafiti kwa lengo la kupata taaluma iliyo bora pamoja na kuelewa mifano ya utafiti kwa kuvitalii na kuvifahamu vipengele vyote vya utafiti kwa kina.

2.2 Maana ya Fasihi Simulizi

Ngure (2003) anasema fasihi simulizi ni sanaa inayotoa maudhui kwa lugha ya maneno ambayo hutamkwa ama hutendwa. Fasihi Simulizi, hupatikana maudhui yake kwa kusikiliza, iwe, maghani au masimulizi, ambayo yana usanii. Mulokozi (1996), anasema, Fasihi Simulizi ni sanaa inayotendwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi. Kwa hivyo Fasihi Simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani ya kijamii na kutawaliwa na mwingiliano wa fanani, hadhira, fani inayotendwa, tukio, mahala na wakati.

Fasihi simulizi ina tanzu kuu nne, ambazo ni; hadithi, semi, maigizo na ushairi. Ushairi ni utungo wa kisanaa ulio na mpangilio maalumu wa lugha ya mkato ambayo

ina fani na maudhui yanayohusu hisi au tukio katika maisha ya mtu katika mazingira au wakati maalumu. Utanzu wa ushairi hujumuisha, mashairi, tenzi, ngonjera na nyimbo. Kwa mnasaba huo nyimbo ni miongoni mwa kitanzu cha fasihi simulizi. kinachoendana na mada ya utafiti huu, kuchunguza maudhui ya nyimbo za kampeni. utanzu huu wa nyimbo, mtafiti, ndiyo aliyofanyia kazi ya kuchunguza maudhui yake. Nyimbo za kampeni, huimbwa wakati maalumu wa kampeni za uchaguzi, pahala maalumu penye uwanja au mazingira maalumu yaliyotayarishwa kwa shughuli hiyo ya kampeni na huimbiwa watu maalumu kwa lengo la kuhamasishwa au kushawishiwa kuhusu uchaguzi. Ili ushairi ukamilike na kuwa na mvuto kwa hadhira, ni vyema kazi hiyo kutungwa na kuwasilishwa kwa kutumia mbinu. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi mazuri ya Luhga, muundo, mtindo, wahusika na mandhari.

2.3 Maana ya Nyimbo

Mulokozi (1996) anafafanua kuwa nyimbo ni kila kinachoimbwa. Mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ni muziki wa sauti ya muimbaji au waimbaji, matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa, muktadha unaofungamana na nyimbo hiyo, kwa mfano, sherehe, ibada, kilio. Fasili hii inafafanua zaidi na kuonesha kusibu katika kazi hii, kwa sababu. Kwenye kampeni za uchaguzi, kuna hadhira maalumu inayoimbiwa, muktadha ambao hufungamana na tukio maalumu la kampeni inayofanyika.

Hamadi (2005) yeye alisema, nyimbo ni sanaa ya lugha, maneno yanayoelezea hisia na fikra, huwa ni teule, yaliyofinyangwa na kusukwa kwa nidhamu na mvuto

unaompendezesha mwimbaji na kumvutia msikilizaji. Fasili hii, imetaja mambo ya msingi ya fasihi, yaani hisia na fikra, mambo haya pia yanapatikana katika nyimbo na hasa nyimbo za kampeni ambazo mtafiti alizifanyia utafiti. Wakati wa kampeni ya uchaguzi, nyimbo huwapa watu hisia kubwa hadi huchanganyikiwa na kufanya mambo kinyume na maadili kama kuvua nguo, kumkataa ndugu wa damu na kuhasimiana na majirani .

Mdungu (2000) anasema, nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Kwa mtazamo wa Mdungu kila kinachotamkwa kwa sauti ya muziki ni nyimbo. Maelezo hayo si lazima yawe sahihi kwa sababu kuna tanzu nyingi za ushairi zenye kutumia sauti za muziki, kwa mfano; mashairi na tenzi za Fasihi ya Kiswahili lakini haziimbiki ila zinaingizwa katika kundi la nyimbo. Kwa maelezo hayo, nyimbo ni tungo za kifasihi zenye mapigo ya sauti au zisizo na mapigo ya sauti ambazo huimbwa kwa madoido, mipumuwo ya sauti, madda, shadda na kuhusisha viungo vya mwili (kwa midengu midogomidogo) ili kukidhi mahitaji na kufikisha ujumbe wa madhumuni yaliyokusudiwa.

Nyimbo ni fani muhimu ya fasihi simulizi katika jamii ya Wazanzibari kwa sababu inatumika katika shughuli mbalimbali za kitamaduni. Shughuli hizo ni kama vile kazi, michezo, sherehe mbalimbali kama vile harusi na mambo ya kijamii kama uganga. Pia nyimbo zina maudhui mbalimbali ya kijamii yakiwemo; kushauri, kuhimiza, kuhamasisha, kuliwaza na kuburudisha. Mdungu (2000).

Wamitila (2006) amesema, Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizo huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya

silabi. Hupangwa kwa utaratibu na muwala wenye mapigo ya kimuziki au mizani. Nyimbo huchukua sehemu kubwa katika sherehe za kijadi za jamii mbalimbali. Maelezo haya yanaonesha kuwa, nyimbo mara nyingi hutumika katika sherehe za kijadi. Fasili hii ya Wamitila inaonesha kuwa nyimbo ni fani maalumu yenye umuhimu mkubwa katika maisha ya kila siku ndani ya jamii. Tuki (2004) wanasema nyimbo (wimbo) ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988) wao wamesema kuwa nyimbo ni utungo wa ushairi wenye mpangilio maalumu wa sauti ya muziki na lugha ya mkato. Nyimbo mara nyingi hutumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Mtandao www.gafkosoft.com/sw/nyimbo (17/06/2015), umeeleza kuwa nyimbo ni aina ya sanaa katika fasihi simulizi ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalumu. Aghalabu nyimbo hutumia ala za muziki kama vile ngoma. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi. Nyimbo hugawanywa katika beti na mishororo, maranyingi nyimbo huwa na kiitikio au mstari ambao hurudiwarudiwa. Maelezo haya yanaonesha kuwa nyimbo ni fani maalumu inayojitafautisha na fani nyengine za fasihi simulizi lakini inalingana na mashairi. Fasili zilizotolewa kuhusu nyimbo, zilitumika ili kukidhi mahitaji ya mtafiti, kwani yaliyofafanuliwa ni muwafaka katika kukamilisha utafiti huu kwa sababu kuna mambo ya msingi juu ya nyimbo kwa sababu, nyimbo huimbwa kwa wakati maalumu, pahala maalumu kutegemea wahusika na tukio lengwa.

2.4 Histori ya Nyimbo

Nyimbo zina historia kubwa katika Ulimwengu huu. Kulingana na wataalamu na watafiti wa fasihi simulizi kama vile Sengo (1978) na Finnegan (1977), wameeleza

kuwa, nyimbo zilianza pale tu binaadamu alipoanza kupambana na mazingira yake katika shughuli za maisha. Hoja hii inafafanua kwamba, chimbuko la ushairi (nyimbo) za Kiswahili ni zao la Waswahili wenyewe kwa sabababu Waswahili wana utamaduni wao ambao ulikuwepo kabla ya ujio wa Waarabu na waliutumia ushairi huo katika shughuli za kijamii kama vile harusi, jando na unyago.

Senkoro (1988) anaongezea kwa kusema katika jamii yoyote maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii huambatana na huenda sambamba na maendeleo ya sanaa ikiwemo ushairi uliotumika katika harakati za maisha ya mwanadamu. Ameendelea kusema kuwa ushairi uliibuka pale lugha ilipoanza katika kipindi cha mwanaadamu alipokuwa anaanza kupata maendeleo kwenda katika kipindi cha mwanaadamu alipokuwa anafanya mambo kwa mantiki ili kumwezesha kupambana na mazingira yake, kwa mfano, kuunda zana za kazi. Zana hizo zilipotumika ziliwafanya waimbe kwa kufuata mdundo wa zana hizo.

Mayoka (1993) anasema ushairi umetokana na jamii ya wanaadamu wenyewe na umesheneza ukwasi mkubwa wa lugha ambayo imekuwa ikitumika katika hatua zote za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, katika historia ambayo mwanaadamu ameipitia tangu enzi za kuishi mapangoni, enzi za uwindaji, ujima, utumwa na maendeleo. Mayoka anaendelea kusema kila jamii ina sanaa yake na ushairi ni moja ya sanaa hizo. Pia ushairi umekuwa na kuendelea kadri jamii inavyokua na kubadilika. Nyimbo ni sehemu ya ushairi wa Waswahili kwa hivyo, utanzu huu wa ushairi, ulianza tangu mwanaadamu alipoanza harakati za kupambana na mazingira yake ili aweze kuishi. Aidha utanzu huu ulibadilika kulingana na mabadiliko ya jamii

katika mifumo mbalimbali ya kiuchumi na kimaendeleo. Ameir (1983) ameongezea kusema, nyimbo ni utanzu wa asili wa fasihi simulizi uliozuka kutokana na harakati na juhudi za binaadamu kuipambana na maisha yao. Nyimbo zilitumika kuwapa nguvu binaadamu wakati wa kazi ngumu kama kuwinda na nyengimezo na kuwaliwaza mabwana na wafalme na kutumika katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Mzee (2011) anasema nyimbo za taarab zilianza kuwepo Zanzibar katika miaka ya 1870 wakati wa kipindi cha utawala wa sultani Sayyid Baraghash Bin Said Visiwani Zanzibar. Katika nyakati hizo inasemekana kuwa nyimbo za taarab ziliingizwa nchini Zanzibar, kama nyimbo za ukumbi za watawala na ziliimbwa kwa lugha ya Kiarabu. Nyimbo hizo zilitumiwa kuwatumbuiza viongozi wenye asili ya kiarabu.

Waimbaji pamoja na ala za muziki ziliingizwa kutoka Misri na Uarabuni. Nyimbo hizo ziliendelea kutumia lugha ya Kiarabu hadi kufikia mwisho wa enzi za utawala wa Sultani Baraghash ambapo lugha ya Kiswahili ilianza kutumika. Mabadiliko haya yanahusishwa na kuibuka kwa mwimbaji wa taarab aliyesifika Zanzibar na nchi za nje, Siti binti Saad mwanamke mwenye asili ya kitumwa. Mzee (ameshatajwa) anasema mnamo miaka ya 1902, nyimbo za taarab zilianza kuenea kwa kuundwa vikundi mbalimbali vya taarab vikiwemo Naad Akhwan safaa (ndugu wapendanao) (1905), Naad Shuub (1910) Royal Air Force (1945) na Michenzani Social Club (1960). Vikundi hivi viliimba nyimbo za kuburudisha watawala, lakini pia vyengine vilitumika kuimba nyimbo za kuelimisha na kuhamasisha umoja wa Waafrika na harakati za kudai uhuru.

Ufafanuzi huu wa historia ya ushairi na nyimbo umesaidia kumfungua zaidi mtafiti katika kuelewa kwamba anapochambua nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar, anazingatia pia suala la historia ya nyimbo ili kupata maudhui yaliyo kusudiwa.

2.5 Sifa za Nyimbo

Nyimbo zina sifa maalumu ambazo hujitokeza wakati wa uimbaji. Bwana Issa Khamis msanii wa kikundi cha Mila na Utamaduni cha Zanzibar, alipozungumza na mtafiti alisema kuwa nyimbo zina sifa zifuatazo:

Hutumia kiimbo au sauti maalumu wakati wa kuimba yaani kupandisha au kushusha sauti, kukaza au kulegeza sauti, kufuata au kutofuata vina; Huweza kuendana na ala za muziki; Huimbwa na mtu mmoja au wengi na wakati mwengine huimbwa kwa kupokezana baina ya mwanamke na mwanamme kama vile nyimbo alizoiimba Sami Haji Dau na Mwapombe Hiyari. Mfano, nyimbo ya Maisha ya vijijini na Mke wa awali ni wewe azizi zilizoimbwa na kikundi cha mila na utamaduni. Nyimbo hizi waliimba kwa kupokezana; Hutumia lugha ya mkato wakati wa kuimba; Hurudia rudia maneno ili kusisitiza ujumbe katika nyimbo hiyo.

Mulokozi (1981) anasema nyimbo huwa na sifa zinazojitafautisha na tanzu nyengine za ushairi sifa hizo ni:

Muziki wa sauti, muziki wa ala, matini au maneno yenye usanii, hadhira inayoimbiwa, muktadha wa nyimbo kama vile sherehe au kazi. Kwa maoni ya mtafiti, sifa zote hizi zilizotajwa zinapatikana katika nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu wa Zanzibar, ambazo mtafiti alizifanyia utafiti ili kupata ufafanuzi sahihi wa kuweza kuainisha nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu.

2.6 Aina za Nyimbo

Kuna aina nyingi za nyimbo miongoni mwa hizo ni; nyimbo za kazi, vita, maadili, malezi, ibada, misiba na kadhalika. Mulokozi (ameshatajwa) amefafanua aina za nyimbo kwa vigezo vya dhima na muktadha. Kutokana na vigezo hivyo, utanzu wa nyimbo umegawanyika katika vijipera vifuatavyo:

2.6.1 Nyimbo za Tumbuizo

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), anasema nyimbo za tumbuizo huimbwa ili kuliwaza au kufurahisha watu kwenye matukio mbalimbali kama misibani, ngomani au harusini. Mfano mzuri ni nyimbo za kubembeleza watoto ambapo kila jamii ina nyimbo hizo.

Nyimbo za kubembelezea watoto huwa na ujumbe ndani yake ambao kwa namna moja hutoa mafunzo kwa walezi na wazazi, TAKILUKI (1982), wamesema kuwa, watoto hawapati mafunzo ya moja kwa moja, lakini hupata maliwazo. Hii inajidhihirisha katika mfano wa wimbo ufuatao ambao ni wa kubembelezea watoto;

Ukilea mwana mwema, na mbaya umlee,
 Huyu ukimsukuma, na huyu umkeme,
 Hujui atakayekufaa, atakayekusaidia baadaye.

Nkwera (1998), ameeleza kuhusu nyimbo za tumbuizo kwa kuangalia katika kipengele kimojawapo cha nyimbo za harusi. Nyimbo hizi kwa asilimia kubwa huwa zimejaa mambo ya mapenzi na ishara mbalimbali zinazowataja wana harusi na maisha ya pamoja na kupendana. Baadhi ya nyimbo huimbwa na watu wazee na wa makamo, nyingine huimbwa na mchanganyiko wa wazee na vijana. Zipo

zinazoimbwa kushangilia tukio la kupokea mahari na zingine huimbwa kushangilia tukio lenyewe la kufunga ndoa.

2.6.2 Kongozi

Mulokozi (ameshatajwa) anasema hizi ni nyimbo za kuaga mwaka. Nyimbo hizi maalumu huimbwa kwa ajili ya kuaga mwaka, hasa mwaka wa kimila. Vigezo vilivyotumika hapa ni kigezo cha kidhima, ambapo dhima yake ni kuaga mwaka na kigezo cha kimuktadha, ambapo muktadha wake ni muktadha maalum yaani huimbwa mwishoni mwa kumalizika mwaka. Mfano mzuri katika sherehe za mwaka kogwa zinazofanyika kila mwaka Makunduchi. Bwana Bakari Gunya mtafitiwa alipokua anazungumza na mtafiti alisema, kila ikifika mwisho wa mwaka tulikuwa tunakwenda mtoni, tunachukua mbao za kusomea chuoni, tukifika, tunazikosha na sisi tunakoga mwaka, njiani huwa tunaimba nyimbo. Wimbo ninaoukumbuka ni:

Letu si letu, la mwalimu wetu

Upanga na mbao, na kalamu zetu

Tunakwenda pwani, kosha mbao zetu

Abdalla kibebeni, kafanya visa njiani

Kasingizia wageni, kombeee jaza.

2.6.3 Nyimbo za Uganga

TAKILUKI (wameshatajwa), wamechunguza na kuona kuwa nyimbo za uganga huimbwa katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na kupiga ramli, kuitia mashetani watu au wakati mwengine kutoa chano kwa mashetani. Shughuli hii hufanywa na waganga wa kienyeji katika viringe vyao wakati wa matibabu kwa

wagonjwa wao. Nyimbo mbalimbali huimbwa wakati wa kuita mashetani, kwa mfano nyimbo ifuatayo huimbwa kwenye ngoma ya Kibundi ambayo ni ngoma ya uganga:

Kina mama msikose mayowe,
 Kwenda tendeje mchana kibandani kwa mtwana,
 Ukitaka nikiatye kanga, siutaki msugunda,
 Siafu wandurume, nduruma siafu.

2.6.4 Nyimbo za Dini

Hizi ni nyimbo zinazoimbwa kwa lengo la kumsifu Mungu au miungu au mitume. Nyimbo hizi huimbwa makanisani, kwenye madrasa na katika maeneo mengine ya shughuli za kidini. Vigezo vilivyotumika ni kigezo cha kidhima ambapo dhima yake ni kumsifu Mungu, miungu au mitume. Pia kimetumika kigezo cha kimuktadha ambapo huimbwa katika muktadha wa kidini kama kwenye shughuli za kidini.

Bi Mwanahawa mtafitiwa alipokuwa akizungumza na mtafiti alisema, kuna nyimbo nyingi za kidini (kaswida) ambazo huimbwa katika madrasa nyingi zilizopo hapa mjini Unguja. Vijana wengi hivi sasa wamerudi kwenye madrasa kwa kufuata nyimbo hizo ambazo siku hizi huingizwa katika ala za muziki, kwa mfano:

Swala tano ndio ngazi,	ya kupandia Peponi,
Yataka tufanye kazi,	tuziswali kwa makini,
Dumisha swala mpenzi,	uziswali swala tano,
Usiifanye ajizi,	adhabu ni kubwa mno,

2.6.5 Wawe

Hizi ni nyimbo za kilimo. Vigezo vilivyotumika ni kigezo cha kimuktadha ambapo huimbwa wakati wa kulima, pia kigezo cha kidhima kimetumika ambapo dhima yake ni kuchapusha kazi. Pia nyimbo hizi huimbwa wakati wa sherehe za mavuno.

2.6.6 Tenzi

Hizi ni nyimbo ndefu za kimasimulizi au mawaidha. Kigezo kilichotumika ni kigezo cha kifani ambapo fani yake ni masimulizi au mawaidha, kwa mfano utenzi wa kisa cha miraji.

2.6.7 Tendi

Hizi ni nyimbo ndefu za masimulizi juu ya matendo ya mashujaa. Vigezo vilivyotumika hapa ni kigezo cha kifani ambapo wahasika wa tendi ni watu wenye historia za matendo ya kishujaa, pia kigezo cha lugha kimetumika ambapo lugha yake ni ya kinathari.

2.6.8 Mbolezi

Hizi ni nyimbo za kilio au maombolezo. Vigezo vilivyotumika katika kugawa kipera hiki ni kigezo cha kimuktadha ambapo huwasilishwa katika muktadha wamaombolezo au kilioni/msibani, pia kimetumika kigezo cha kidhima ambapo dhima yake ni kuomboleza kwenye misiba au maafa.

2.6.9 Kimai

Hizi ni nyimbo zihusuzo shughuli za baharini. Vigezo vilivyotumika hapa ni kigezo cha kidhima ambapo dhima yake ni kuchapusha kazi. Vilevile katika kigezo cha

kimuktadha, kimai huwasilishwa katika mazingira ya baharini. Wavuvi wakati wako kwenye harakati zao za uvuvi huimba ili kujifariji na kujipa nguvu za kuvua, wasichoke, wasitegeane ili uvuvi ufanyike vizuri na kwa ufanisi.

2.6.10 Nyiso

Nyimbo hizi huimbwa katika mazingira maalumu ya porini, au sehemu nyengine zilizo maalum za jando, dhima yake ni kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu maisha ya utu uzima. Vile vile nyimbo hizi huwasilishwa katika mazingira maalumu yaliyotayarishwa kwa ajili ya jando au unyago.

Kungwi mwambie mwario,	asiache ufunguo,
Akiacha ufunguo,	atafungua mwenzio.
Kungwi mwambie mwario,	asiache kuvipika,
Akiacha kuvipika,	watavipika wenzio.
Kungwi mwambio mwario,	asiache kusafisha,
Akiacha kusafisha,	watasafisha wenzio.
Kungwi mwambie mwario,	asiache kutandika,
Akiacha kutandika,	watatandika wenzio.
Kungwi mwambio mwario,	asiache bembeleza,
Akiacha bembeleza,	tabembeleza wenzio.

2.6.11 Nyimbo za Vita

Nyimbo hizi zinaimbwa na askari wakati wa vita. Lengo la nyimbo hizi ni kuwahamasisha askari na kuwapa moyo wa ushindi wazidi kupigana, wasichoke, wasikate tamaa, wala wasivunjike moyo.

Adui akija,	sisi tuko tayari,
Akija aridhini,	kanyaga kanyaga kanyaga sisi tuko tayari,
Akija angani,	tungua tungua tungua sisi tuko tayari,
Akija baharini,	zamisha zamisha zamisha sisi tuko tayari.

2.6.12 Nyimbo za Kazi

Mulokozi (amesha tajwa), anaona kuwa nyimbo za kazi ndilo kundi kubwa zaidi. Karibu kila kazi ifanywayo na watu huwa na nyimbo zake kama kilimo, uvuvi (kimai), uwindaji, useremala, kutwanga, kupepetu, kusuka, kuchuuza, uashi na ufuaji chuma. Senkoro (1987), anafafanua kuwa wimbo wa kazi humpa mtu nguvu na ari zaidi ya kuendelea kufanya kazi.

2.6.13 Nyimbo za Uwindaji

Wawindaji wakati wa shughuli za kuwinda au sherehe zao baada ya mawindo huimba, nyimbo hizi ambazo huimbwa na makundi ya wawindaji, hulenga kuwaburudisha baada ya kazi ngumu waliyofanya au huimba ili kujipa moyo na kujihamasisha wakati wa uwindaji.

2.6.14 Nyimbo za Watoto

Watoto wana michezo mingi, michezo hiyo ya watoto hutawaliwa na nyimbo. Zipo nyimbo nyingi zinazoimbwa na watoto wakati wa michezo yao. Mara nyingi wakati wa jioni, magharibi na usiku, watoto hukusanyika mitaani, hucheza na kuimba. Nyimbo hizo zinakuwa na lengo kuu la kuburudisha lakini wakati mwengine huwa na maana kubwa katika malezi. Mdungi (2000).

TAKILUKI (1983), wamesema nyimbo za michezo ya watoto zinaonekana hazina maana kamili, lakini huimbwa ili zilingane na mshindo na mpangilio wa mchezo. Ziko baadhi ya nyimbo zina maana kamili na kuwa zinatoa mafunzo fulani. Mfano mzuri ni wimbo wa saka mke wangu ambao huimbwa na watoto wanawake peke yao au wakati mwingine huimbwa na wanawake na wanaume. Wimbo huu hutoa funzo kwa wanawake na wanaume waliooana kuagana wakati wanapokwenda safari ili kuzidi kujenga mapenzi. Wimbo huo ni;

Saka mke wangu	saka mke wangu.
Hapa hayupo	hapa hayupo.
Kenda wapi	kenda wapi.
Kenda kwa msusi	kenda kwa msusi.
Ruhusa kampa nani	ruhusa kampa nani.
Kampa msusi	kampa msusi.
Shanuo kampa nana	shanuo kampa nani
Kampa msusi	kampa msusi
Hapa nitaukata	haukatiki
Hata kwa panga	haukatiki
Kwa msumeno	haukatiki
Yasisi yankaranga sia ya sisi yankaranga sia	

Mulokozi (ameshatajwa) anasema kuwa michezo ya watoto imeficha itikadi ya jamii kuhusu mahusiano. Kwa mfano, wimbo wa mchezo wa “Kachiri” humfundisha mtoto wa kike kustahimili shida wakati mumewe anaposafiri. Kwa mfano wimbo unasema:

Kachirii kachiri	saga
Mume wangu kasafiri	saga
Kaniachia ukili	saga
Upatao pima mbili	saga
Nakipande cha hariri	saga
Hapata kuku hamkaranga	kwa pilipili na dawa ya manga
Kachiri saga kachiri saga	kachiri saga saga saga

2.6.15 Nyimbo za Taifa

Hizi ni nyimbo za kusifia Taifa au kabila. Kila Taifa huwa na wimbo unaolitambulisha Taifa au kabila au wimbo wenye kusifu Taifa, kabila, au mtu mwenye historia kubwa katika Taifa hilo. Dhima kubwa ya nyimbo hizi kusifia Taifa au kabila, kujenga na kuimarisha uzalendo. Kwa mfano wimbo wa kumsifu mwalimu Nyerere:

Twanza tangu awali kumsifu msifika
 Julius mkamili bingwa aliye ongoka
 Mtanzania kamili mwananchi mzalika
 Nyerere Raisi mwema mwenye busara na hekima.

2.6.16 Nyimbo za Siasa

Hizi ni nyimbo zinzoimbwa katika harakati za siasa kama vile kampeni za uchaguzi, mikutano ya vyama vya siasa. Nyimbo hizi zinadhima ya kuburudisha na kuhamasisha wanachama, viongozi na wapenzi wa vyama vya siasa. Kwamfano;

Tunataka nchi yetu sasa tumechoka
 Tafrani hii tafrani hii

Tunataka nchi yetu sasa tumechoka

Tunataka tunataka wee

Shida nyingi shida nyingi wee

Tunataka nchi yetu sasa tumechoka

Katika utafiti huu, aina hizi za nyimbo zilimsaidia mtafiti katika uainishaji wa nyimbo kutambua zipi nyimbo za kampeni za uchaguzi na zipi si nyimbo za kampeni.

2.7 Fani Katika Nyimbo

Ili kazi ya fasihi iweze kutoa maudhi yake na kuwafikia walengwa kama ilivyokusudiwa na kuwa na mvuto kwa wasomaji au wasikilizaji wake ni vyema kazi hiyo itungwe kwa kuzingatia fani. Katika fani kuna vipengele ambavyo vinaijenga fani hiyo, miongoni mwa vipengele hivyo ni matumizi mazuri ya lugha, muundo na mtindo mzuri, ambao utaifanya hadhira kuwa na hamu ya kujua hatma ya kazi husika, uumbaji mzuri wa wahusika, pamoja na mbinu nyingine mbalimbali za uandishi.

2.7.1 Utangulizi

Fani ni mbinu au ufundi anao buni na kutumia mtunzi wa kazi ya fasihi ili kufikisha kwa hadhira ujumbe aliokusudia John na mduda (2011). Fani ina kamilika kwa vipengele mbalimbali ambavyo ni wahusika, lugha, muundo, mtindo na mandhari. Wamitila (2004) amesema, fani katika kazi ya fasihi ni ufundi anaoutumia msanii kuwasilisha kazi hiyo kwa jamii. Fani hujumuisha lugha yenye usanii, wahusika walioumbwa kulingana na uhusika wao, muundo, mtindo na mandhari.

Omary (2011) anasema, fani ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mtunzi wa kazi ya fasihi katika kuisanii kazi yake. Ufundi huo wa kisanaa unapatikana katika vipengele vya wahusika, muundo, mtindo, matumizi ya lugha na mandhari katika kazi ya fasihi. Wamitila (2008) na msokile (1992) wanasema ufundi huo wenye usanii katika kazi ya fasihi, huwavutia wasomaji na wasikilizaji wakati wanaposoma au kusikiliza kazi hiyo ya fasihi.

2.7.2 Vipengele vya Fani

Msokile (ameshatajwa) anasema vipengele vya fani katika kazi ya fasihi ni vile vipengele vinavyo jenga umbo la kazi ya fasihi. Mara nyingi vipengele hivyo huwa ni pamoja na muundo, mtindo, mandhari, wahusika na lugha. Si lazima vipengele hivyo kujitokeza kwa uzito ule ule katika kila kazi ya kifasihi. Msokile (ameshatajwa) anaendelea kusema katika mashairi ya nyimbo, fani hujumuisha vipengele vifuatavyo:

Muundo; Ni mjengeko wa ushairi. John na Mduda (2011) wanasema muundo ni mjengeko au sura ya nje ya shairi inayotegemezwa kwenye mfuatano wa idadi ya beti, mpangilio wa vina na urefu wa mishororo (mistari) inayofuatana kwa kutegemea mtiririko wa wazo au hisia iwapo ni shairi huru. Ushairi wa fasihi simulizi una miundo mbalimbali. Nyimbo nyingi huwa na viitikio, beti zake huweza kuwa na idadi ya mishororo (miistari) inayotafautiana. Urefu wa beti aghalabu hutegemea idadi ya mishororo. Kwa ufupi muundo ni umbo la nje la shairi la nyimbo. Kipengele hiki kiliweza kumsaidia mtafiti kujua muundo wa nyimbo za kampeni katika lengo la kuainisha nyimbo hizo.

Mtindo; Ni kipengele cha fani ambacho msanii hutunga kazi na kuipa uzuri kifani na kimaudhui. Mtindo huambatanishwa na tabia ya mtungaji ambayo humpambanua mtunzi mmoja kutokana na mwenziwe. Katika muktadha huu, mtindo hubainika kutokana na namna mtunzi anavyojieleza kwa kutumia lugha na mbinu nyengine za kisanaa, mafumbo au kufumbata ujumbe kwenye urefu au ufupi wa sentensi zake. Aidha dhana ya mtindo hujumuisha wasanii wa kipindi fulani cha historia na sifa zao za uandishi. Kipengele hiki kilimsaidia mtafiti katika lengo la tatu la kutafuta mbinu za kuzifanya nyimbo za kampeni kuleta umoja badala ya utengano.

Wahusika; Ni viumbe vyenye uhai au visivyo uhai vinayotenda katika kazi ya fasihi ambavyo huwakilisha ubinaadamu, mashairi ya nyimbo hayatumii sana wahusika katika kuwasilisha ujumbe, mara nyingi wahusika wake huwa ni waimbaji na wasikilizaji. Mtafiti amekitumia kipengele hiki katika utafiti wake ili kuonesha kwa namna gani waimbaji na wasikilizaji wanavyo changia kuibua maudhui ya nyimbo.

Lugha: Katika mashairi lugha ina nafasi kubwa. Mashairi ya nyimbo nayo hutumia lugha yenye mpangilio maalumu wa maneno yaliyoteuliwa ili kuwasilisha ujumbe wake. Msokile (ameshatajwa) amesema; lugha ya kishairi hujivimbisha kiasi cha kuvuta nadhari za wasomaji au wasikilizaji.

John na Mdunda (2011) wanasema ushairi wa fasihi simulizi una miundo mbalimbali. Mathalan, viitikio na beti zake huwa na idadi ya mishororo (miistari) inayofanana au inayotafautiana.

Abeid (1973) anasema mashairi ya Kiswahili yana mitindo mingi, kuna mashairi ambayo hufuata urari wa vina na mizani na mengine hayafuati urari huo. Kuna

mengine yana vibwagizo, mengine hayana. Kuna mengine hutumia mizani nane nane kwa kumi na sita na mengine hutumia nusu mistri. Kwa hiyo urefu wa mistari yake unaweza kutafautiana kutegemea idadi ya mezani zilizotumika katika mstari huo.

2.8 Mapitio ya Maandishi

Mtafiti aliwaangalia wataalamu, Welling (2000). Patrick (2003). Andrews (1993) na Opie (2010) ambao wameelezea uandishi wa pendekezo la utafiti na ripoti ya utafiti kwa kufafanua namna ya kuandika utangulizi, kuchagua mada ya utafiti, namna ya kuandika usuli wa mada. Pia, wamefafanua kuhusu tatizo na usuli wa tatizo. Vipengele hivi vimemsadia sana mtafiti kupata taaluma ya kufanya utafiti na kuandika ripoti ya utafiti. Lengo na madhumuni wameyafafanua na kumuwezesha mtafiti kupata mwongozo mzuri wa kukamilisha utafiti. Baada kutalii kazi hizo, mtafiti aliingia ndani kwenye bahari ya akili. Kutafuta ukuwaji na upatikanaji wa taalimu na elimu. Akavitalii vitabu vya saikolojia. Hapa mtafiti alitaka kujuwa vipi akili na tabia za watu hukuwa na hubadilika ili apate mwongozo wa kumsaidia kufanya utafiti wake. Mtafiti aliwaangalia wataalamu Santrock (2003). Malim na Birch (1998) na Child (2004). Katika kazi hizi, mtafiti amepata mwongozo mzuri wa uchambuzi wa nadharia, muongozo ambao ulimsaidia sana katika kazi yake hii. Baadae, mtafiti aliingia kwenye wataalamu wa nyimbo. Huko aliwatalii wafuatao:

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2007), ambao wamezungumzia utamaduni wa Wazanzibari. Nyimbo ni sehemu ya utamaduni, lakini waandishi hao wamezigusa nyimbo kwa kiasi kidogo sana. Na nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu wa Zanzibar hazijaguswa kabisa. Utafiti huu ulitarajia kuzitafuta na kuzifafanua kwa urefu majukumu ya maudhui ya nyimbo hizo.

Mdungu (2007), Msokile (1972), Simiyu (2011), Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (1983), Taasisi ya ukuzaji mitaala (1988), John na Mdunda (2011), wamezungumzia nyimbo kama utanzu wa Fasihi Simulizi, unaohifadhiwa kichwani, pia wamezungumzia fani na maudhui ya mashairi. Mtafiti aliweza kupata ufafanuzi uliomsaidia kujua kwamba nyimbo za kampeni ya uchaguzi ni sehemu ya fasihi simulizi, zenye fani na maudhi na lengo la kuburudisha na kuelimisha jamii. Katika nyimbo walizozielezea na aina walizozitaja, nyimbo za kampeni za uchaguzi hazikuelezwa, wakati zina maudhui makubwa kwa ustawi na maendeleo ya jamii ya Wazanzibari. Utafiti huu umekusudia kufichua majukumu ya dhamira hizo.

Sheriff (1991), Nasser (1999), wamezungumzia historia nzima ya tawala za kikoloni na wafalme waliyotawala Zanzibar. Zanzibar hiyo ya asili ilikuwa ni mwambao wote wa Afrika Mashariki kuanzia Kaskazini Somalia mpaka Kusini Ruvuma, vikiwemo visiwa vyake na miji yote kama Mogadishu, Barawa, Kismayu, Pate Lamu, Malindi, Mombasa, Bwagamoyo, Pangani, Unguja, Pemba, Tumbatu, Kilwa, Mafia na miji mengine ya mwambao huo. Kwa wakati huo ilijulikana kuwa ni dola ya Zanzibar.

Naseer (ameshatajwa) anasema miji hii ilianza kuvamiwa na kutekwa na Wareno mnamo miaka ya 1500. Mnamo mwaka 1729 Wareno hao waliondoshwa kwa kupigwa na watu wa Afrika Mashariki walioshirikiana na Waarabu wa Omani. Naseer aliendelea baada kutolewa Wareno, Zanzibar iliingiliwa na Waarabu kutoka Oman kwa kipindi kirefu. Waarabu hao walianza kuingia kama wafanyabiashara baadae wakahodhi maeneo mengi na kuanzisha tawala zao za kifalme

Sayyid Said bin Sultani mwaka 1804 mpaka 1856

Sayyid Majid bin Said mwaka 1870 mpaka 1888

Sayyid Khalifa bin Said mwaka 1888 mpaka 1890

Sayyid Ali bin Said mwaka 1890 mpaka 1893

Sayyid Hemed bin Thuwain mwaka 1893 mpaka 1896

Sayyid Khalid bin Baraghash 1896, huyu alitawala kwa kuvamia, alikaa kwa muda mfupi kabla ya kuondoshwa kwa nguvu na Uingereza mwaka huohuo 1896.

Sayyid Humoud bin Muhamed mwaka 1896 mpaka 1902

Sayyid Ali bin Humoud mwaka 1902 mpaka 1911

Sayyid Khalifa bin Harub mwaka 1991 mpaka 1960

Sayyid abdalla bin Khalifa mwaka 1960 mpaka 1963

Sayyid Jamshid bin Abdallah mwaka 1963 mpaka 1964 alipokimbia kwa Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964. Mbogo (2015) alisema wakati wananchi wakisherehekea uhuru wa Zanzibar mwaka 1963, vijana wa kiafrika wakiongozwa na John Okelo hawakuutambua uhuru huo na wakasema huo ni uhuru wa bandia, kisirisiri wao walikuwa wakijiandaa na mapinduzi. Azma yao hiyo ya mapinduzi waliitekeleza mwezi mmoja tu baada ya uhuru huo tarehe 12 /01/1964.

Kwa mtafiti wa kazi hii, maelezo hayo yalimsaidia kujua historia ya Zanzibar, kuanzia tawala za jadi, wageni na wenyeji walipoingia Zanzibar, tawala za kifalme, mivutano ya kuwania mamlaka na madaraka, vita vilivyopiganwa Zanzibar na sababu zake, chaguzi mbalimbali, uhuru na mapinduzi ya Zanzibar. Mtafiti alipata kujuwa namna kampeni zilivyokuwa zikiendeshwa na nyimbo zilivokuwa zikitumika kwenye kampeni hizo. Kwa kiasi kikubwa, wataalamu hao waliweza kumsaidia mtafiti kupata historia kamili ya Zanzibar.

Seif (2011), ameeleza, kwa kina, kuhusu nyimbo za unyago katika jamii ya Kikaguru. Ameeleza kuhusu dhima za nyimbo zinazoimbwa katika unyago. Ni kukuza mila na dasturi za Wakaguru. Mtafiti alitafiti nyimbo za unyago tu zinazotowa mafunzo ya unyumba, ambazo zinakuza malezi katika jamii ya Kikaguru. Kazi hiyo imemsaidia mtafiti wa kazi hii kuweza kujua aina za nyimbo, dhima za nyimbo, na maarifa yaliyomsaidia kufanya utafiti wake vizuri zaidi. Pili, kuona mwanya uliopo, wa kumuwezesha mtafiti, kujua zaidi hatua za uandishi wa utafiti wake.

Juma (2007), amezungumzia matumizi ya lugha na mitindo katika nyimbo za uganga. Ameeleza zaidi mitindo ya lugha iliyotumika katika uganga. Lugha ya uganga inakuwa ni tafauti na lugha ya kawaida, lugha hii huwa na sauti nzito yakutisha yenye ukali kwa sababu huwa ni ya kuitia shetani, na shetani wengine ni wakaidi kwa hivyo hulazimika kutumika lugha hiyo. Mtafiti wa kazi hii amefaidika kujua kuwa kila nyimbo ina mtindo wake wa lugha kulingana na madhumuni ya nyimbo hiyo. Pia mtafiti ameweza kujua umuhimu wa matumizi ya lugha katika nyimbo, elimu aliyopata hapa ilimsaidia kufanya kazi yake vizuri.

Abdalla (2011) ameeleza athari za mabadiliko katika nyimbo za taarab. Katika utafiti wake ameeleza namna nyimbo za taarab zilivyokuwa zikiimbwa na zinavyoimbwa hivi sasa. Amesema zamani nyimbo za taarab zilikuwa hazichezwi kama zinavyochezwa siku hizi, haziimbwi kama zinavyoimbwa siku hizi. Shairi la wimbo wa taarab hufumbwa, haliachwi wazi kama inavyofanywa leo. Mawazo kama haya yametolewa na Abeid (1973) amesema moja kati ya sifa kubwa ya mashairi ni

lugha yenye usanii ambayo haiko wazi wazi. Mawazo haya yamemsaidia mtafiti wa kazi hii kutambua tafauti ya lugha zinazotumika katika mashairi. Pia aliweza kutambua sababu za matumizi ya lugha ya waziwazi na lugha za mficho, kwa mtafiti wa kazi hii ilimsaidia sana kuweza kuifanya kazi yake vizuri.

Gora (2011), ameelezea nyimbo za uganga wa pepo. Nyimbo hizo huimbwa kwa kuitia pepo au kufurahisha pepo anapopewa chano. Haziimbwi pahala pengine zaidi ya kiringeni. Tasnifu hiyo ilimsaidia mtafiti kupata maarifa ya kujua mbinu na hatuwa za kufuatwa wakati akifanya utafiti wake. Vile vile, tasnifu hii ilimuwezesha mtafiti kuona upungufu uliopo. Simai (2005) ameeleza mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za harusi katika ndowa za Unguja. Katika tasnifu hiyo ameonesha namna nyimbo zinavyotumika katika kutoa mafunzo ya unyumba. Mwanamke ameelekezwa kukaa na mume wake na vipi mume anatakiwa kukaa na mke wake. Katika utafiti alioufanya, nyimbo, za kampeni za uchaguzi hakuzigusa. Mtafiti wa kazi hii ameweza kuona pengo hilo baada ya kutalii tasnifu hiyo. Ameweza kupata taaluma ya utafiti .

Salum (2010) ameelezea mchango wa nyimbo za unyago katika kumkomaza mwari kiunyumba Wilaya ya Kinondoni. Katika tasnifu hiyo mtafiti alichambua nyimbo zinazoimbwa unyagoni kwa lengo la kumkomaza mwari ili aweze kuimiliki nyumba, yaani kukaa na mume, kumuhudumia mume na watoto. Nyimbo hizo zina mafunzo mengi, kubwa ni kazi moja tu ya kumfunda mwari. Kwa mtafiti wa kazi hii, amepata maarifa ya uandishi wa pendekezo na ripoti ya utafiti yaliyomsaidia katika kukamilisha utafiti wake.

Haji (2013), ameelezea nafasi ya hadithi simulizi ikiwa ni utanzu wa fasihi simulizi katika kufunza maadili mema, skuli za sekondari Zanzibar. Hadithi hizo zina nafasi kubwa ya kufunza maadili mema. Alisisitiza zitumike katika kutatua matatizo. Kwa mtazamo wa Haji, fasihi simulizi ikitumika vizuri hutatua matatizo ya jamii. Baada ya kuisoma kazi hii, mtafiti alipata kuelewa kuwa fasihi simulizi ina michango mingi ndani ya jamii, miongoni mwa michango hiyo ni kutatua matatizo yanayojitokeza katika jamii. Maarifa haya yalimsaidia mtafiti katika lengo lake la tatu la kutafuta njia na mbinu za kuzifanya nyimbo za kampeni kuleta umoja katika jamii ya Wazanzibari. Kwa hivyo kazi hiyo ilikuwa ni msaada mzuri katika kukamilisha kazi yake, hasa kwakua nyimbo za kampeni ni sehemu ya fasihi simulizi ambayo ilikuwa haijafanyiwa utafiti.

Daud (2012), amezungumzia kuhusu nyimbo za daku, kila jamii ina utamaduni wake. Nyimbo za daku ni sehemu ya utamaduni wa watu wa Zanzibar ambao siku hizi unasahaulika. Siku hizi Nyimbo hizo hazisikiki zikiimbwa wakati wa Ramadhani. Nyimbo hizo zilileta umoja na upendo ndani ya jamii. Kazi hiyo ilimsaidia mtafiti kujua kuwa Nyimbo zilileta umoja na upendo ndani ya jamii. Kwa hivyo alihamasika kutaka kufanya utafiti huu ili aweze kujua kuhusu nyimbo za kampeni.

Said (2005), alizungunzia kuhusu mafunzo yanayopatikana katika nyimbo za michezo ya watoto wadogo Unguja. Katika kazi hiyo amegundua kuwa nyimbo za watoto zina umuhimu mkubwa, katika kukuza vipaji vya watoto, kuwa na uwezo wa udadisi, kuelewa na kukuza utamaduni wao ushirikiano na upendo miongoni mwao

na maelewano. Ameendelea kusema, mafunzo yanayopatikana yanasaidia kumkuza na kumlea mtoto kiakili. Lakini jamii ya watu wa Zanzibar haijatilia maanani nyimbo hizo. kazi hiyo imemsaidia mtafiti kuona umuhimu wa nyimbo katika jamii. Hivyo kumpa nafasi ya kutafiti nyimbo za kampni za uchaguzi mkuu Zanzibar.

Badru (2012), ameelezea kwa kina kuhusu taswira zilizomo katika nyimbo za taarab. Pia ameelezea athari za matumizi ya taswira katika nyimbo za taarab. Kwa mtazamo wake, ameona watu wengi wamechunguza maudhui ya nyimbo za taarab. Yeye akaamua kuchunguza taswira. Pamoja na kuifanya kazi yake, bado maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar, hazikuwamo katika utafiti wake. Mwanya huo ndio aliutumia mtafiti huyu katika kuazimia kufanya utafiti huu. Aidha mtafiti wa utafiti huu, alipata maarifa yaliyomsaidia kukamilisha utafiti huu kwa wepesi.

Mzee (2011) amezungumza mengi kuhusu athari za nyimbo za mipasho katika maisha ya watu wa Zanzibar. Amesema, nyimbo za mipasho za taarab zimeathiri kwa kiasi kikubwa mwenendo na tabia za watu wa Zanzibar, hasa vijana. Athari hizo zimeonekana kwenye vipengele vya utamaduni hasa maadili na uhusiano wa watu, tabia zao, ndoa zao, mapenzi yao na nyendo zao. Kwa hivyo, amependekeza kuwe na bodi ya sensa ili kudhibiti nyimbo zenye maadili mabaya. Nyimbo hasa alizochunguza ni nyimbo za taarab za mipasho. Nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu wa Zanzibar hazijachunguzwa. Pengo hili ndilo lililopelekea mtafiti wa kazi hii kupata shauku ya kufanya utafiti huu. Pia mtafiti amepata maalumati mengi yaliyomsaidia kukamilishia kazi yake hii.

2.9 Mkabala wa Nadharia

2.10 Maelezo ya Dhana Muhimu

Nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo mkuu wa mtu au watu (jamii) wa pahala fulani, wakati fulani kwa sababu fulani. Sengo (2009). Owhida (2006) anaeleza kuwa nadharia yaweza kuwa ni mawazo ya mtu au kundi la watu kuhusu jambo fulani ambalo linaweza kuwa la kweli au la dhahania, aghalabu linaweza kuwa na mwelekeo wa watu, jamii, kundi au mtu na kusaidia kupata ukweli au hata kuthibitisha ukweli wa jambo kwa lengo maalumu. Nadharia ni mawazo yanayotumika kuwa ni mwongozo wa kutekeleza jambo au kutambulikana dhana. Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010) Kwa maelezo haya, nadharia ya utafiti ni mwongozo wa kufuata wakati wa kufanya utafiti wa kazi za fasihi ili kuonesha njia, kanuni, na maelekezo ya kufuata katika utafiti huo. Kuna nadharia nyingi ambazo hutumiwa na wahakiki na watafiti wa kazi za fasihi ili kuwaongoza katika kazi zao. Mtafiti alitumia nadharia chache kati ya hizo ili kumuongoza, na kumrahisishia ukamilishaji wa utafiti huu, nadharia hizo ni:

2.10.1 Nadharia ya Mtu na Utamaduni

Hatch (1976) katika nadharia hii ya mtu na utamaduni, amelezea nadharia hii katika hali tatu, kwanza, kihistoria: utamaduni hutoka pahala fulani na kupokewa pahala pengine na kubadilishwa kulingana na mazingira ya pahala husika.

Pili, utamaduni huzuka kutokana na mwongozo wa kisiasa na haki za kumiliki mali. Tatu, mifumo ya dini, itikadi na kazi za hayo katika kujenga na kuimarisha jamii tulivu yenye mshikamano. Utamaduni ni ustaarabu, kwa hivyo hudhibiti mambo

ambayo mtu hufasiri maumbile na mazingira yake. Kwa mtazamo huu kila jamii ni lazima iwe na utamaduni ambao huwakilisha mazingira halisi ya jamii pamoja na mabadiliko ya kihistoria. Utamaduni pia huonekana ni nyenzo ya kimsingi ya mabadiliko ya mtu katika harakati zake za maisha.

Nadharia hii ni muhimu katika utafiti huu, kwa sababu inaonesha kuwa kuwepo kwa utamaduni kunategemea kuwepo kwa mtu, kama mtu hayupo na utamaduni haupo na jamii isiyo na utamaduni, haina utulivu, kwa hivyo utulivu na mshikamano wa jamii unategemea utamaduni. Basi, mtu na utamaduni haviwezi kutengana. Kila kitu kina asili yake. Nadharia hii imesaidia mtafiti katika uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za kampeni.

2.10.2 Nadharia ya Fasihi ina Kwao

Sengo (2009) anaeleza kuwa, mtu kuelewa fasihi ya fulani ni lazima ajuwe eneo linalohusika, utamaduni wao, mila zao, dasturi zao, lugha yao, mazingira yao. Fasihi ya Kiswahili kwao Uswahilini, pwani, mwambao wa Afrika ya Mashariki, ambako kuna jadi zao, katika viambo vyao, makaazi yao, katika vijiji vyao na miji yao. Kwa mtazamo wa Sengo, fasihi za duniani kote si sawasawa, ijapokuwa kuna baadhi ya mambo hulingana. Kwa mtazamo wa nadharia hii mtu huasisi utamaduni na utamaduni humtambulisha mtu kutokana na kuwa kila jamii ina mambo yake, ustaarabu wake, desturi zake, ada zake na kawaida zake. Utamaduni ni pamoja na sanaa, na sanaa huunda fasihi, na fasihi ni pamoja na nyimbo. Nyimbo ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Nadharia hii imesaidia mtafiti katika uchambuzi wa maudhui kuweza kujua tabia ya matusi ilitokea wapi? Pia iliweza kumsaidia mtafiti kubaini

mbinu za kuzifanya nyimbo za kampeni zielimishe na kuleta umoja badala ya kuleta mivutano na utengano.

2.10.3 Nadharia ya Tabia

Pavlov (1936) na Skinner (1938) ambao ni waasisi wa nadharia hii wanaeleza kuwa nadharia hii inajikita katika imani kuwa binaadamu na viumbe wengine wote hai wana kitu kiitwacho tabia. Kila kiumbe hujifunza tabia. Kitu hiki hazaliwi nacho bali hujifunza mara tu azaliwapo. Tabia ina pande mbili, kuna tabia nzuri na tabia mbaya. Tabia zote hizi hutegemea kiumbe huyo kajifunza kutoka wapi, au kutoka kwa mwalimu gani.

Tabia ndiyo inayotenganisha wanadamu na wanyama. Mtu akiwa na tabia mbaya huambiwa hakupata mwalimu mzuri na huwa chini kuliko mnyama. Athari za maisha ya watu wenye tabia mbaya ni rahisi sana kuigwa na watoto. Binadamu hutakiwa kuwa na tabia nzuri. Kwa mtazamo huu inakuwa ni wajibu wa mzazi kumfunza na kumuongoza mtoto wake ili awe na adabu nzuri na tabia nzuri.

Pia Santok (2001) ameongezea kuwa, tabia imejengeka vipande vipande. Mtu mwenye kuvipanga vipande hivyo mpaka vikakaa pamoja na kuwa kitu kizima, mtu huyo husemwa ana tabia nzuri, na ndiye mwenye kupata maendeleo. Nadharia hii imemsaidia mtafiti, kujua nyimbo zenye kufunza tabia nzuri na mbaya, ambazo hurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Vilevile nadharia hii imeweza kumsaidia mtafiti katika uchambuzi wa data kuona sababu za wanajamii kufanya mambo kwa kufuata mkondo na upepo, kutunga na kuimba nyimbo zenye kuleta utengano badala ya kuleta umoja.

2.10.4 Nadharia ya Uhalisia

Hegel (1975,1979) alisema neno uhalisia lina maana ya kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Uhalisia ni kuifanya kazi ya kubuni inayotokana na ulimwengu wa wanaadamu kwa kutumia lugha inayofahamika.

Nadhari hii ilianza kutumika katika fasihi kule Ufaransa katikati ya karne ya kumi na tisa, na baadae ilisambaa Uingereza, Urusi na Marekani. Morris (2003) aliendelea, nadharia hii, ilizuka kama njia moja ya watu kupinga ulimwende, mambo ya kilimwende yaliyokuwa ya kinjozi zaidi yasiyowezekana kutendeka.

Wavula na Njoge (2001) wanasema kwamba nadharia hii ndio muhimu zaidi kutokea katika karne ya kumi na tisa na ishirini na pengine itaendelea kutuathiri. Nadharia hii imehusisha miktadha miwili. Kwanza, inatumiwa kama njia ya kutathmini hali. Huu ni uhalisia wa maisha. Uhalisia wa fasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Maana ya pili ndiyo iliyotumiwa huko Ufaransa mwaka 1850 kuelezea kazi ya sanaa inayoonesha maisha ya binaadamu jinsi yalivyo. Uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anapopatikana mwanaadamu. Wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia hii waliamini kuwa, dhima ya msanii ni kuonesha ukweli jinsi ulivyo.

Wavula na Njoge (wameshatajwa) wanaendelea kusema, imani ya wahalisia ni kuwa, kazi za fasihi zinafaa kuwafanya wanaadamu katika dunia yao ya kawaida ya ukweli na uhakika na halisi. Kwa hivyo picha za dunia watakazochora wasanii ni lazima

kuonesha kazi hiyo. Wananadharia hii wanasisitiza kwamba msanii anawajibu kuteuwa lakini akiwa na nia ya kutekeleza maswala yake kama yanavyo husu watu katika hali halisi ya maisha.

Wamitila (2006) anasema, uhalisia, kwa kiasi kikubwa, huichukulia kazi ya fasihi kuwa inahifadhi au kuakisi hali halisi ya maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unaweka mkazo kwenye uwasilishaji wa mambo yanayotoka katika jamii. Kwa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa. Pia kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii.

Nadharia hii, imemsaidia sana mtafiti wa kazi hii, kwa sababu msanii wa nyimbo za kampeni za uchaguzi alitakiwa kutunga nyimbo zenye uhalisia wa mambo yalivyo katika jamii yenye ukweli. Kwani mambo haya ndiyo yatakayopelekea wanajamii kupata uamuzi sahihi wa yale watakayoyaamua baada ya kampeni. Pia ukweli ungeliswaunganisha wanajamii zaidi kuliko kuwatenganisha. Nadharia hii, pia inajifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaopatikana katika maisha halisi, wahusika hao huchunguza, husimulia maisha na tajiriba zao, kusawiri na kuonesha mandhari na mazingira ya kawaida. Kwa hivyo msingi mkuu wa nadharia hii ni masimulizi.

Ndani ya utafiti huu, nadharia ya Uhalisia, imetumika, katika uchambuzi wa data, umefanywa kwa kuzingatia msingi wa nadharia hii. Mtafiti ametumia nadharia hii kutokana na msingi wake mkuu ambao ni masimulizi ya ukweli na uhalisia.

Muhusika husimulia matukio kama yalivyotokezea au kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Mtunzi wa nyimbo za kampeni ni miongoni mwa wahusika, kwa hivyo alihitajika kutunga nyimbo zenye uhalisia wa mila na utamaduni wa jamii ya Wazanzibari ili kulinda maadili.

Kutokana na msingi huo, tunapotaka kufafanua, maudhui ya nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu Zanzibar, hatuna budi kuyaangalia maisha halisi na mahusiano yake na vipengele hivi vya fasihi. Nadharia hii inayaelezea maisha kwa uhalisia wake, kwa kuonesha, binadamu anatoka wapi, yupo wapi na anaelekea wapi? Kwa msingi huo nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu Zanzibar zina mwelekeo huo. Vipi binaadamu anaweza kupambana na mazingira katika jamii yake yakamtoa katika hatua moja duni na kumpeleka katika hatua nyengine iliyo bora. Licha ya kwamba, baadhi ya wanajamii husema kuwa, nyimbo hizo zinatoa hamasa, jazba na kusababisha mivutano katika jamii.

Nadharia hii pia inatoa mwelekeo katika vipengele vya fani vifuatavyo:

- (i) Muundo na muwala katika kazi ya fasihi.
- (ii) Wahusika na lugha wanayotumia.

Vitu hivi, kama vinavyo fafanuliwa na nadharia hii ya Uhalisia, vinasisitiza uchambuzi wa kazi za fasihi kama zao la jamii, kwa hivyo, mtafiti vilimsaidia kuonesha ukweli wa maisha kama ulivyo katika uchambuzi wa maudhui. Kwa ujumla kila nadharia ina nafasi yake katika kazi ya mtafiti. Hakuna nadharia iliyojitosheleza peke yake katika kukamilisha kazi hii.

2.11 Hitimishi

Kwa ujumla, sura hii imezungumzia mapitio mbalimbali yaliyotumika katika utafiti huu. Nadharia zilizotumika, na kubaini nadharia ambazo ni mnasaba zilizomuongoza mtafiti huyu katika utafiti wake. Pia imegusia tafiti tangulizi kuhusu nyimbo hizo. Sura inayofuata inaelezea mbinu za utafiti na vifaa vilivyotumika katika utafiti huo.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu. Sura hii ina sehemu sita. Sehemu ya kwanza ni mkabala wa utafiti. Sehemu ya pili, eneo lililotumika kwenye utafiti. Sehemu ya tatu, mbinu za ukusanyaji wa data. Sehemu ya nne, uteuzi wa watafitiwa na namna walivyopatikana. Sehemu ya tano, ukusanyaji wa data na sehemu ya sita, zana za kukusanyia data.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mkabala usio wa kiidadi. Enon (1998) na White (2000) wameelezea mkabala huu kuwa ni njia ya ukusanyaji wa data inayolenga kukusanya data kwa njia ya maelezo na data zinazopatikana haziwakilishwi kwa tarakimu. Mkabala huu unafaa zaidi kutumika katika utafiti wa masuala yanayohusu sayansi ya jamii, kama fasihi. Hii ni kwa sababu mkabala huu haufungwi sana na kanuni na unaweza kutumika sambamba na njia nyengine kama hojaji na usaili.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar, katika kisiwa cha Unguja, Mkoa Mjini Magharibi Wilaya ya Mjini, kwa sababu ni sehemu inayokusanya watu kutoka sehemu zote za Visiwani na ni sehemu inayoanzisha mambo yote. Unguja mjini ni kituo na kitovu cha mambo yote muhimu ya maisha na uendeshaji wa uongozi na utawala wa Serekali. Mtafiti alipata baadhi ya data alipotembelea ofisi za Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) zilizokuwepo Mwanakwerekwe, Wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi.

3.4 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni hatua za kitaalimu za mtafiti, ambazo zinakuwa kulingana na kazi ya mtafiti, na namna alivyokusanya data, kuzichambuwa na kuziandikia taarifa yake. Bailey (1994), Mgogo (2012) wanasema mbinu ni namna mtu anavyoweka mikakati ya kufanikisha jambo lake. Kwa maelezo hayo mbinu za utafiti ni fani maalumu anayoitumia mtafiti ili kumsaidia kukusanya data zilizosahihi katika utafiti wake.

Katika kazi hii mtafiti ametumia mbinu zaidi ya moja kukusanyia data ili kukamilishia utafiti wake. Zipo sababu mbalimbali ambazo zilimfanya mtafiti kutumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data. Kwa mujibu wa Kothari (2004) anasema mtafiti huamua kutumia mbinu za utafiti zaidi ya moja. Hivyo basi, katika utafiti huu sababu zilizopelekea kutumia mbinu za kukusanyia data zaidi ya moja ni kupata data ambazo zisingelipatikana kwa kutumia njia moja peke yake. Kwa malezo ya Kothari ameshatajwa hakuna mbinu iliyobora katika utafiti ikitumika peke yake. Ni vyema kukusanya data kutoka katika vyanzo na mbinu mbalimbali ili mtafiti aweze kuhakiki matokeo kupitia mbinu hizo. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu zifuatazo:

3.4.1 Mbinu ya Maktabani

Mtafiti alitumia maktaba kusoma maandishi mbali mbali yenye mnasaba wa mada hii ambayo kwa (namna moja ama nyingine) yaliunufaisha utafiti wake. Mtafiti alitumia Maktaba za Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Baraza la Kiswahili Zanzibar, Baraza la Sanaa Zanzibar, Maktaba Kuu ya Zanzibar, Chuo Kikuu Huriya cha Tanzania, Idara ya nyaraka na mambo ya kale Zanzibar, Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam pamoja na maktaba ya Idara ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtafiti aliweza kusoma vitabu, tasnifu, na majarida mbalimbali yenye kuafikiana na mada. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata kilichofanywa na watafiti waliopita ili kubaini pengo lililopo na kuliziba kwa namna anayoona inayofaa.

3.4.2 Mbinu ya Masikanini (Makaazini)

Enon (1998), na Sengo (2011) wameeleza kuwa, hii ni mbinu ya ukusanyaji data, kwa mtafiti kushiriki. Huishi maskanini na jambo analolichunguza ili kukusanya taarifa anazozihitajia. Mtafiti alitumia mbinu ya masikanini ili kupata data za msingi kutoka kwa watafitiwa. Mbinu hii ilimsaidia sana mtafiti kutafsiri data iliyotokana na yeye kuona, kuhisi, kusikia data walizozionesha waimbaji wakati wakiimba na kuitikia. Hii inatokana na ukweli kwamba wasanii huonesha hisia za furaha kwenye furaha, hisia za jazba na mori katika mazingira husika.

Mbinu hii pia ilimuwezesha mtafiti kukutana na kuwahoji watu ambao, kwa namna moja ama nyingine, ni wapenzi wa nyimbo za kampeni za uchaguzi, wakiwemo wasanii, wapenzi na hata wataalamu wa masuala ya fasihi na utamaduni. Fursa hii ilimuwezesha mtafiti kukutana na kujadiliana nao juu ya maudhui yanayojitokeza katika nyimbo hizo za kampeni.

3.4.3 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mpangilio mzima wa mfano wa maswali yenye lengo la kutafuta data au taarifa kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana kwa kutumia maswali ya mitindo tofauti tofauti, Kothari (2009). Mtafiti aliwasaili watu wenye ujuzi na utaalumu, kuhusu nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu Zanzibar, wakiwemo wataalamu

mbalimbali, na wapenzi wa nyimbo hizo. Mtafiti alifanya nao usaili wa ana kwa ana, akapata maarifa zaidi yaliyomsaidia kutanua wigo wa utafiti huu.

Faida kuu ya usaili ni kwamba, mtafiti huchukua maelezo ya moja kwa moja na ya kuaminika kutoka kwa mtafitiwa, pia maelezo hayo yamemsaidia kuthibitisha taarifa zenye mashaka. Taarifa hizo zilipatikana kwa watu wa aina zote, waliosoma na wasiosoma. Kwa upande wa utafiti huu, mtafiti aliwasaili watafitiwa ambao ni wanataaluma katika fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu ch Taifa (SUZA), Skuli za Sekondari Lumumba, Hamamni, mwembeladu na Vikokotoni.

Mtafiti aliandaa maswali yaliyomuongoza katika usaili huo. Kupitia mbinu hii mtafiti pia alifanya usaili na watafitiwa wengine wakiwemo wasanii wa nyimbo za kampeni, wanachama wa vyama vya siasa, waandishi wa habari na watu wazima. Mbinu hii ilikuwa ngumu kidogo kwa watafitiwa, kwa sababu wengi wao walikuwa hawajiamini vizuri, walijibu kwa wasiwasi kidogo. Hata maoni yao waliyatoa kwa tahadhari wasije wakakosea.

3.4.4 Mbinu ya Hojaji

Hojaji ni mbinu ya utafiti anayoitumia mtafiti kutafutia data. Kothari (2004). Anafafanua kuwa, mbinu hii huhusika uandaaji wa hojaji ambayo hutumwa kwa mtafitiwa na ombi la kumtaka kujibu maswali yaliyomo katika hojaji hiyo na hatimaye kurudishwa kwa mtafiti. Hojaji hiyo huhusisha orodha ya maswali ambayo huwekwa katika mpangilio na utaratibu maalumu. Katika utafiti huu mtafiti aliandaa maswali mengi ili kuwapa uhuru na nafasi watafitiwa kujibu kwa uhuru na kuelezea hisia, uzoefu na maarifa waliyonayo juu ya mada husika.

Sababu ya kuamua kutumia mbinu hii ni kwamba, mtafitiwa huwa yuko huru kuelezea hisia zake, mawazo na maoni yake juu ya jambo fulani kwa uwazi. Kwa hivyo mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data za kutosha na kwa uwazi zaidi kwa kuwapa watafitiwa nafasi ya kuelezea mawazo, hisia, mtazamo na uzoefu wao.

3.4.5 Watafiti Wasaidizi

Mtafiti alitumia mbinu ya kuwa na watafiti wasaidizi kutokana na mazingira ya ukusanyaji wa data yalivyo. Kwanza, mtafiti alilazimika kwenda kwenye vikundi vya taarabu na ngoma ambako mtu asiyehusika haruhusiwi kuingia. Mtafiti alilazimika apate watafiti wasaidizi, watakao muwezesha kufika ndani ya vikundi hivyo na kupata siri za utungaji na uimbaji wa nyimbo za kampeni.

Pili, mtafiti alihitaji kuwapata watu wazima, waandishi wa habari na wataalamu wa lugha ya Kiswahili ili aweze kukutana na watafitiwa hao, alilazimika apate watafiti wasaidizi aliyesaidiana nao kupata wenyeji wa kukutana na watafitiwa hao. Vile vile ni vigumu kukutana na wanasiasa ambao hawakujui, watafiti wasaidizi walichukua jukumu la kumtambulisha mtafiti na kuweza kufanya mahojiano na viongozi wa kisiasa na kujaza hojaji.

Njia hii, ilimsaidia mtafiti kupata data za uhakika kwa wepesi, lakini wakati mwengine ilimnyima uhuru mtafiti katika vikundi vya wanasiasa kwa sababu katika maeneo mengine, alilazimika mtafiti msaidizi kujibu au kuuliza maswali kwa kuwaridhisha wanasiasa kinyume na utaratibu wa mtafiti. Vilevile wakati mwengine mtafiti hakuruhusiwa kuingia katika vikundi vya ngoma bila ya kuwa pamoja na mtafiti msaidizi.

3.5 Uteuzi wa Watafitiwa

Watafitiwa lengwa, ni wale ambao mtafiti aliwateuwa akiwa na imani, watampatia data itakayomuwezesha kukamilishia utafiti wake, New Man (2006). Kombo na Tromp (2006) wamesema, walengwa ni kundi wakilishi la watafitiwa linaloweza kutoa majibu ya maswali ya mtafiti. Webster (1985) anasema, walengwa ni kikundi cha watu wachache kilichoteuliwa kutoka katika kundi la watu wengi kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. Katika utafiti, walengwa wanaweza kuwa wakulima, wavuvi, watumishi wa umma, madereva, walimu, watoto, vijana au mtu yoyote mwenye taarifa zinazohitajiwa na mtafiti.

Uteuzi wa watafitiwa hufanywa kwa kuteuwa kikundi kidogo kinachowakilisha kundi kubwa la watu ambalo linafanyiwa utafiti, Cohen na wenzake (2001), Minduva (2004), wanafafanua zaidi kuwa, kikundi kidogo kinachoteuliwa, huwakilisha kundi kubwa linalofanyiwa utafiti kwa sababu, si rahisi kufanya utafiti ukachukua jamii nzima ya watu wanaotafitiwa.

Utafiti huu umetumia mawazo hayo pamoja na Kothari (2008) na Opie (2010) ya kuwateuwa watu kuwakilisha jamii ya Wazanzibari. Uteuzi wa kikundi hicho kidogo cha watu, ulifanywa kwa kutumia mbinu yenye madhumuni maalumu na dhamira zinazohusisha uteuzi wa watu ikiwa ni sampuli inayofanywa na mtafiti kutegemea taarifa zinazohitajika katika utafiti.

Watu wote hao walichaguliwa kwa kutumia mbinu ya kukusudia ili kupata maelezo ya kina na ya usahihi. Utafiti ulitarajiwa ufanywe kwa kutumia watafitiwa mia moja

na kumi (110) Kati ya hao, wanaume walikuwa hamsini na watano (55), na wanawake hamsini na tano (55). Idadi hiyo ndogo ya watu ilikuwa ya watafitiwa waliosaidia kufanikisha utafiti huu. Watu hao ni vijana, watuwazima, walimu, wasanii, wasomi, wataalamu wa lugha ya Kiswahili na waandishi wa habari kama inavyoonekana katika jedwali namba 3.1.

3.5.1 Vijana

Kundi hili, lilijumuisha wale vijana wakike na wakiume wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 ambao hawasomi skuli, (waliosoma wakatoroka au wasiopelekwa kabisa) ambao hawafanyi kazi maalumu. Vijana hawa wapo katika Wilaya ya mjini, katika maeneo ya shehiya ya Chumbuni, Makadara, Malindi, Mkunazini na shehiya ya Shaurimoyo.

Mtafiti aliteua kundi hili kutoka katika shehiya hizi kwa sababu ndilo kundi linalofuata mambo na matokeo yanayotokea kutokana na kuwa halina kazi maalumu ya kufanya, kwa hivyo kundi hilo ndilo linaloshiriki zaidi katika kuimba na kuhudhuria katika kampeni. Katika maeneo haya, aliyoyachagua mtafiti anategemea kupata data sahihi kwa sababu yapo maeneo yenye mivutano mikubwa kama vile Malindi, Chumbuni na Mkunazini. Pia kuna maeneo ambayo hayana mivutano mikubwa, kama vile Mlandege na Shaurimoyo.

3.5.2 Watu Wazima

Kundi hili linajumuisha wazee wanaume na wanawake, wenye umri kati ya miaka 45 na 65. Kundi hili lilituliwa na mtafiti kwa sababu ni watu waliojua mengi na walioona mengi, na liliwashirikisha watu maarufu, weledi wa mambo ya kisiasa

katika jamii. Mtafiti alifanikiwa kuwashirikisha watu kumi na saba, kumi na wawili kati yao walijaza hojaji na watano alifanya nao mazungumzo ya ana kwa ana. Mtafiti aliweza kupata mawazo mengi na maoni mbalimbali yaliyosaidia katika utafiti huu.

3.5.3 Walimu

Kundi hili la walimu lilipatikana katika skuli tafauti, zilizopo katika Wilaya ya Mjini. Miongoni mwa hizo ni, Skuli ya Sekondari Lumumba, walimu sita. Wanawake watatu na wanume watatu, Skuli ya Sekondari Hamamni, walimu wawili mmoja mwanamme na mmoja mwanamke, Skuli ya Sekondari ya Mwembeladu, walimu wawili, mmoja mwanamke na mmoja mwanamme.

3.5.4 Wasanii

Kundi hilo la wasanii wa sanaa ya taarab, waandishi wa kazi za fasihi, wasanii wa ngoma za asili, watunzi wa nyimbo, waimbaji, waitikiaji na viongozi wa vikundi hivyo vyote. Kundi hilo, limeteuliwa kutokana na kuwa wote hao kuhusika moja kwa moja na mada hii. Mtafiti, ameweza kukusanya data muhimu kupitia watafitiwa hao. Watafitiwa wengine walijaza hojaji, na wengine walifanya mahojiano maalumu ya ana kwa ana na Mtafiti.

3.5.5 Wasomi

Kundi hili lilijumuisha wanawake na wanaume wenya elimu ya shahada ya kwanza, ya pili na ya juu zaidi. Mtafiti alilichagua kundi hili kwa sababu, ni kundi lililochambua maudhui ya nyimbo kitaalamu. Mtafiti alipata mchango mkubwa katika ukusanyaji wake wa data kutoka kwa wasomi, mchango huo ulimsaidia kupata data sahihi za kuaminika zilizo msaidia kukamilisha utafiti wake.

3.5.6 Wataalamu wa Lugha ya Kiswahili

Kundi hili la Wataalamu wa Lugha ya Kiswahili, lilikuwa ni muhimu kwa mtafiti. Kwa sababu, lilichambua nyimbo za kampeni kisanii. Kundi hili liliwajumiisha wataalamu kutoka Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA). Mtafiti alipata ufafanuzi wa nyimbo alizozitumia katika utafiti huu.

3.5.7 Waandishi wa Habari

Kundi hili la waandishi wa habari, lilipatikana kutoka Shirika la Habari la Zanzibar (ZBC), kundi hili lilijumuisha, waandishi wa redio na wa tivii, wanawake na wanaume. Kundi hili la waandishi wa habari, lilikusika moja kwa moja na mada hii kwa sababu, kampeni zote zilizofanyika, waandishi wa habari walihudhuria ili watowe habari kwa jamii. Kundi hili lilikuwa muhimu sana, kwa sababu lilikuwa likihudhuria kampeni zote, lilisikia na kuona nyimbo za vyama vyote. Kwa mtafiti, kundi hili lilimsaidia sana kukusanya data zilizo muwezesha kukamilishab utafiti wake.

Jedwali Namba 3.1: Jumla ya Watafitiwa

WAHUSIKA	W'ume	W'wake	Jumla
Vijana	10	10	20
Watu wazima	05	05	10
Walimu	10	10	20
Wasanii	05	05	10
Wasomi	10	10	20
Wataalamu wa lugha ya Kiswahili	10	10	20
Waandishi wa habari	05	05	10
JUMLA	55	55	110

Chanzo: Mtafiti (2015)

3.6 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data katika utafiti huu, ulifanywa kulingana na utaratibu uliobuniwa na mtafiti. Jumla ya watafitiwa 85 walipatikana kati ya 110 waliotarajiwa. Kwanza, mtafiti alifika katika maeneo husika ya watafitiwa akiwa na vifaa vyake vya kukusanyia data, kama vile, kalamu, kitabu cha kuandikia, simu na vyenginvyo. Mathalan skuli, kwanza alijitambulisha kwa Mwalimu Mkuu, akamkabidhi barua iliyomruhusu kufanya utafiti, baadae alikutana na mwalimu wa somo la Kiswahili ambae alikuwa ni miongoni mwa watafitiwa aliyefanyanae mahojiano.

Aidha katika vikundi vya taarabu, ngoma na maeneo mengine ya maskanini, mtafiti aliongozana na mtafiti msaidizi, ambae alikubali kuchukua dhamana ya kumfikisha mtafiti katika maeneo yaliyokuwa magumu kufika peke yake na kuweza kukusanya data, katika vikundi vya ngoma na matawi ya vyama vya siasa hasa vya upinzani, hapo mtafiti alikutanishwa na watafitiwa na alianza kukusanya data ambazo ndizo zilizomsaidia kukamilisha utafiti huu.

3.7 Zana za Kukusanyia Data

Zana na vifaa vya kukusanyia data ni jumla ya vifaa vilivyomsaidia mtafiti kukusanya na kuhifadha data alizozikusanya kwa mujibu wa mtandao wa www.raqualia.com>Research and Development uliotembelewa tarehe 19/07/2014 umefafanua kwamba zana za kukusanyia data ziko za aina nyingi sana ambazo hutumika katika aina mbalimbali za tafiti zikiwemo tafiti za kisayansi, kitaaluma, kifasihi na nyenginezo. Zana hizo ni pamoja na kompyuta (ngamizi), daftari na kalamu, kinasa sauti na kadhalika.

Ili kufikia lengo la utafiti wake, mtafiti katika utafiti huu, alitumia mashine za kidigitali katika kurekodia data alizozipata kutoka kwa watafitiwa wake, kwa mfano, alitumia kinasa sauti kurekodi, kisha akarekodi sauti. Vifaa vilivyotumiwa ni pamoja na kamera ya video, kinasa sauti na simu ya mkononi. Mtafiti alivitumia vifaa hivyo kurikodia ili aweze kusikiliza tena na tena kwa ajili ya kupata usahihi wa taarifa alizozikusanya. Mtafiti aligundua kuwa vifaa hivyo ni muhimu kwa kuwa viliweza kumrahisishia ukusanyaji wa data ya nyimbo ambazo huimbwa na huwa si rahisi kwa mwimbaji kurudia sauti na maneno yale yale. Lakini matumizi ya vifaa hivyo yalimfanya mtafiti kukusanya data nyingi, kwa watafitiwa wengi na kwa wepesi zaidi. Mtafiti alitumia kompyuta, daftari na kalamu, kinasa sauti na simu. Vifaa hivi vilimsaidia mtafiti, kuweka kumbukumbu vizuri wakati alipokuwa akikusanya data.

3.8 Hitimishi

Kwa jumla, sura hii imeangalia mkabala wa utafiti uliyotumika eneo la utafiti, mbinu na zana za ukusanyaji wa data katika utafiti, pamoja na uteuzi wa watafitiwa wa utafiti. Sura hii imechambua namna mbinu hizo zilivyotumiwa na namna gani ziliweza kumsaidia mtafiti kukamilisha utafiti wake. Sura inayofuata itakuwa ni uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amewasilisha data na kuzichambua ili kutoa taarifa halisi ya kile kilichowasilishwa kupitia data hizo. Aidha, majadiliano kuhusiana na data zilizokusanywa yalitolewa kwa lengo la kuweka bayana majibu ya utafiti huu. Kwa hivyo, mtafiti amefanya uchambuzi wa data za awali na taarifa alizokusanya kutoka katika eneo la utafiti. Data alizowasilisha ni zile alizoziona kuwa ni muhimu katika utafiti huu.

Utafiti uliongozwa na lengo kuu la kuchunguza na kuchambua maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu katika jamii ya watu wa Zanzibar, kuanzia mwaka 2000 hadi 2010 katika kustawisha jamii ya watu wa Zanzibar. Madhumuni maalumu yalikuwa ni:

- (i) Kukusanya na kuainisha nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar 2000-2010.
- (ii) Kutathmini mchango wa nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar katika kusitawisha jamii ya Wazanzibari.
- (iii) Kutafuta mbinu za kuzifanya nyimbo hizo ziwe zinaleta umoja badala ya utengano katika jamii ya Wazanzibari.

Ili kutimiza madhumuni haya, maswali matatu yaliulizwa na kupata data toshelevu.

Maswali hayo yalikuwa ni:

- (i) Ni nyimbo gani, hutumika katika kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar?

- (ii) Jee nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar zina mchango gani katika kustawisha jamii ya Wazanzibari?
- (iii) Ni mbinu zipi zinazoweza kutumika ili nyimbo za kampeni za uchaguzi, mkuu wa zanzibar zisaidie kuimarisha chaguzi hizo ili kuleta umoja kwa Wazanzibari badala ya utengano?

Malengo haya yamefikwa kwa kiasi kikubwa, hasa kwa vile yaliweza kupima kile kilichokusudiwa. Hali hii ilimsaidia mtafiti kupata tafsiri halisi kwa kila data iliyokusanywa na namna ilivyoweza kupima lengo lililokusudiwa na mtafiti.

Uwasilishaji, uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo katika utafiti huu vimepangwa kwa kufuata mtiririko wa malengo maalumu na maswali yake kama ifuatavyo:

4.2 Kukusanya na Kuainisha Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar 2000-2010

Katika lengo hili, mtafiti alikusanya na kuzichambua nyimbo ishirini na tatu (23) kutoka katika vikundi sita, kikundi cha kwanza ni kikundi cha mila na utamaduni, katika kikundi hicho mtafiti alikusanya nyimbo tano ambazo ni uchaguzi, amani, Rabi twaomba salama, demokrasia na Mola ibariki nchi yetu. Kikundi cha pili ni kikundi cha sanaa cha Mkoa Mjini Magharibi. Katika kikundi hicho, mtafiti alikusanya nyimbo nne ambazo ni baba Bilali, naangurume, wakaanga mbuyu na mama Kikwete. Kikundi cha tatu kilikuwa ni kikundi cha Imarisha, katika kikundi hicho, mtafiti alikusanya nyimbo tano ambazo ni komando Salmini, Tanzania,

balahau, hamwishi kuzua na hongera hongera. Kikundi cha nne ni kikundi cha uhamasishaji cha Chama Cha Wananchi (C.U. F), katika kikundi hicho, mtafiti alikusanya nyimbo tatu ambazo ni chaguo letu ni wewe mwalimu Seifu Sharifu, helwa helwa na chereko chereko. Kikundi cha East African Melody, kilikuwa ni kikundi cha tano. Katika kikundi hicho, mtafiti alikusanya nyimbo nne ambazo ni wasohaya wana mji wao, njangu hata wewe, fisadi kiwembe na kinyangunya. Kikundi cha sita ni Tanzania one theater. Katika kikundi hicho, mtafiti alikusanya nyimbo mbili ambazo ni harambee harambe mama harambee na pisha njia.

Nyimbo za kampeni za uchaguzi zilizokusanywa na mtafiti zikiwa ni sehemu ya fasihi simulizi, huburudisha, hubomoa maadili, huleta na huondosha umoja wa Wazanzibar, hudumaza mila na utamaduni na husababisha migogoro katika jamii.

Kuburudisha: Wasanii wa nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, hutunga na kuimba nyimbo ili kuwaburudisha wanachama wakati wa mikutano ya kampeni. Wakati wanachama wapo kwenye mikutano wakisubiri viongozi wao kuwahutubia, nyimbo mbalimbali huimbwa kwa madhumuni ya kuwaburudisha ili wasichoke kusubiri na wakati mwingine huimbwa ili wasichoke kusikiliza kwa mfano wimbo wa mama Kikwete na baba Bilali. Bi Mwanahawa mtafitiwa alisema baadhi ya nyimbo za kampeni huimbwa ili kuwaburudisha watu waende katika mikutano ili wasichoke kukaa wakiwa wanawasubiri viongozi. Watu huimba, hucheza na hufurahi. Kwa mfano wimbo wa Mola ibariki nchi yetu, Rabi twaomba salama na muungano. Mola ibariki nchi yetu ni mfano mzuri wa wimbo ya kuburudisha.

Mola wetu ya manani	ibariki nchi yetu
Izidi kuwa amni	tukuze uchumi wetu
Amani kitu muhimu	hili tunalitambua
Hata kwa mwenda wazimu	amani huhitajia
Seuze watu adhimu	akili zilotulia
Seuze watu adhimu	akili zilotulia
Amani kwa wanadini	huabudu kwa utuo
Padiri na makuhani	huhubiri kwa matao
Shekhe na wanavyuoni	hutulia na ya kwao
Shekhe na wanavyuoni	hutulia na ya kwao
Amani kwa wakulima	hulima kwa kutulia
Hawalimi na kuhama	mazao kuyakimbia
Huvuna tena kilima	kila siku ikingia
Huvuna tena kilima	kila siku ikingia
Amani ikipotea	kuitafuta ni taabu
Hata kule kusinzia	kwa mtu huwa ajabu
Balaa itaingia	amani yetu dhahabu
Balaa itaingia	amani yetu dhahabu

Kuhamasisha: Nyimbo za kmpeni huimbwa katika mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa lengo la kuwahasisha wanchama na wengine wanaokwenda kwenye mikutano ya kampeni. Nyimbo hizo huwavuta watu kutoka majumbani mwao.njiani

na maskanini kwenda kwenye viwanja vya mikutano. Nyimbo huhamasisha watu kujiandikisha na kupiga kura, wakati mwingine huhamasisha watu kuwachukia wafuasi wa chama chengine. Bi Kipini mtafitiwa msanii alisema, watu walikuwa huja mikutanoni ili kusikiliza nyimbo zetu, watu hao hucheza huhamasika sana na hawakosi kuja katika mikutano kusikiliza kuna nyimbo gani mpya. Nyimbo zilizokuwa zinawagusa zaidi ni zile zilizokuwa zinawapa hamasa viongozi na kuwasema viongozi wa vyama vya upinzani. Kwa mfano wimbo wa naangurume, Komando Salmi, hongera hongera, nyimbo hizi zikiimbwa watu hupanda jazba, huhamasika sana. Pia nyimbo za chaguo letu ni wewe maalim Seif Sharifu, chereko chereko na heluwa heluwa, nyimbo hizi zikiimbwa wanachama wa chama cha wananchi popote walipo huacha shughuli zao wakaanza kusikiliza. Vilevile za harambee, pisha njia, uchaguzi, kwa wanachama wa chama cha mapinduzi huwahamasisha sana katika uchaguzi na kuwafanya wanavyama kuwapenda sana viongozi wao, vyama vyao, na wengine kuchukia. Komando Salmi ni mfano mzuri wa nyimbo ya kuhamasisha.

1. Ndugu wapinzani wanasema turudi ya zamani

Mji mwisho mikunguni na kangili ziwe Pemba mjini hizo

CCM we imeshika usukani, inazidi kwenda mbele na nahodha Komando Salmi.

2. Mapinduzi mwayalani sera zenu kutoka Arabuni

Miti yote iko chini mmejenga mpaka Magogoni

CCM we imeshika usukani, inazidi kwenda mbele na nahodha Komando Salmi.

3. Kina mama mfikiri cha CUF sio chama chenu
CCM ni hodari yasomesha hao watoto wenu
CCM we imeshika usukani, inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmin.
4. CUF imevaa tai kiunoni wamefunga herizi
Nyumba waloweka tawi ni faida ya Mapinduzi
CCM we imeshika usukani, inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini.
5. Komando kaanza kazi kwenye kipindi kigumu
Alofanya yako wazi tumpongeze kwa mashamsham
CCM we imeshika usukani, inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini.
6. Mapinduzi mwa yalani sera zenu za kishetani
Maendeleo hamuoni mmeganda nyumba za Michenzani
CCM we imeshika usukani, inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini.

Kiitikio:

Komando ndo dereva uyoo	Tumempenda wenyewe
Wabaya cheka nao	Tumempenda wenyewe
CUF awapa chajio hao	Tumempenda wenyewe

Mila na utamaduni: Ndani yake tunapata maadili, nyimbo zina lengo la kujenga na kuimarisha mila, utamaduni na kudumisha maadili mema katika jamii kwa kutumia lugha nzuri na kushauri malezi bora katika jamii. Nyimbo za kampeni mara myingi zinaenda kinyume na lengo hili.

Bwana Khatibu Mchenga mtafitiwa alisema, nyimbo nyingi za kampeni zinachangia sana kuvunja maadili ya jamii yetu. Kwa mfano wimbo wa fisadi kiwembe, kinyangunya na balahau. Lugha iliyotumika katika nyimbo hizi inakwenda kinyume na maadili ya jamii ya kizanzibari, kwa mfano wimbo balahau ubeti wa tatu:

Baba Amani usijibu	tutajibu kina mama
Uyo kiongozi wao	na bi Kipini kafanana
Sidiria hafu twaazimana	japo kuwa langu pana

Kwa maelezo ya watafitiwa wengi akiwemo mwalimu Masoud Yakoub, Bakari Gunya, Latifa Iddi walisema utamaduni wa Wazanzibari tangu asili na jadi ni umoja na mashirikiano, kuishi kidugu, kula pamoja na kushiriana katika shughuli zote za kijamii. Nyimbo za kampeni za uchaguzi zinasababisha umoja wa makundi kwa sababu kila chama huimba na kusifu upande wao na kukashifu upande mwengine.

Kwa mfano wimbo wa wakaanga mbuyu hamwishi kuzua, Njangu hata wewe na wasohaya wana mji wao, wimbo wa wasohaya wana mji wao ni mfano mzuri unaoonesha jinsi watu na makundi yanayokashifiana upande mmoja na kuonesha dharau kubwa kwa upande mwengine, wimbo unasema:

Binaadamu waso haya wana mji wao ,
Hawana lililo baya kwa upande wao,
Jambo wakikutendea nisawa sawa kwao,
Waallahi masikini roho zao.

Wazuri sura jamali maumbile yao,
Kumbe ni watu thakili tabia zao,
Huchunga na kusaili mambo ya wenzao,
Waso haya wana mji wao.

Yao huyaficha mbali vibindoni mwao,
Kweli wasohaya wana mji wao,
Warambaji visogoni watu wa namna hao,
Majungu na kufitini ndio kazi yao.

Tonge yako kwenda kinywani hawapendi wao,
Hata ukiwathamini huna jema kwao,
Wasohaya hawajali utu wao ,
Wasohaya wanafanana hata sura zao.

Kupuliza na kutafuna ndio kazi zao,
Nyuso wameshazichuna kwa umbea wao,
Wenyewe wanajuana wana mji wao,
Naona yatawashinda ni hasara kwao.

4.3 Kutathmini Michango ya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu, Zanzibar Katika Kustawisha Jamii ya Wazanzibar

Katika kufikia lengo hili, mtafiti alizifanyia tathmini nyimbo za kampeni alizozikusanya na michango ya watafitiwa mbalimbali ambao walielezea jinsi nyimbo hizo zinavyoweza kustawisha jamii ya Wazanzibari.

Mtafiti baada ya kufanya tathmini hiyo aligundua kwamba, nyimbo za kampeni za uchaguzi wa Zanzibar zina mchango mkubwa wakati wa kampeni, mingoni mwa michango yake ni; kuburudisha, kuhamasisha jamii wakati wa mikutano ya kampeni, na kutoa ajira.

4.3.1 Kuburudisha

Moja ya majukumu ya fasihi ni kuburudisha. Watafitiwa wengi wameeleza kuwa, nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu wa Zanzibar, zinaburudisha na kuwatia hamasa wananchi kwenda kushiriki katika uchaguzi. Wakati wa burudani hiyo nyimbo zinashajihisha jamii, zinawataka watu kupiga kura wakati ukifika, kuchukua fomu za kupigia kura na kumchagua mtu anaye takiwa. Bi mwanaisha Mnemo Othman (Bi Kipini) msanii maarufu wa Kikundi cha ngoma cha Imarisha alisema, nyimbo za kampeni zilikuwa zikitoa burudani kubwa wakati zikiimbwa. Watu huja kuzisikiliza nyimbo hizo tu, zikimalizika, wao huondoka kwa mfano: Nyimbo ya Muungano niliyoimba mwenyewe aliimba:

Tanzania muungano nchi mbili

Tanganyika na Zanzibar

Tumesha ungana sie

Twamkumbuka baba Nyerere

Kutuunganisha kuku bali nchi yake

Baba kuibadilisha

Bila wasi wasi baba yetu Karume

Alikubali muasisi muungano usimame

Tena sote kwa pamoja tulifurahi sana

Muungano ni mmoja sasa tumetulizana

Tuyashike pamoja muungano kutumia.

Jumla ya watafitiwa 80 walisema kuwa Nyimbo hizo za Kampeni zinaburudisha jamii

4.3.2 Kuhamasisha

Nyimbo za kampeni zinahamasisha jamii na kuishawishi ikubaliane na mawazo ya wanaopiga kampeni. Kwa hivyo, nyimbo zinatumiwa kuwavuta na kuwashawishi watu. Bi Khadija Issa Hatibu, mwandishi wa Habari wa Shirika la Habari la Zanzibar (ZBC), akizungumza na mtafiti, alisema, nyimbo za kampeni zinawavuta watu na zinawafurahisha. Lengo kuu ni kuhamasisha jamii. Vile vile, Bi Mtumwa Foum Juma, mzee, mtafitiwa mwenye umri wa miaka 58, yeye alisema, anapenda kuzisikiliza nyimbo za kampeni kwa sababu zinamvutia na zinamgusa sana mfano; wimbo wa uchaguzi, demokrasia, na amani. Mfano mzuri ni wimbo wa uchaguzi,

Tutie tutie kwa moyo mmoja

Nambari one eeeee

Nambari one ni CCM

Lengo kuu, ni kuihamasisha jamii ikapige kura na ichague CCM lakini aliongezea kusema, nyimbo hizo za siku hizi, hazina ufundi mkubwa, tafauti na zile nyimbo zao walizokuwa wakiimba zamani, kwa mfano nyimbo za zamani zilikuwa hufumba zinapendeza zaidi, kwa mfano;

Fundi wangu nimakuja

Unichongele kidayu

Nimpakile mjomba

Yeye na mkaza hayu

Mkoloni kenda mbio

Hata shati kasahayu.

Kiitikio

Simba ukimuulia mwanawe

Machango humnguruma

Ukuisikia parakacha

Haingiliki mrima.

Huu ni wimbo waliokua wanaimba zamani wako watoto katika ngoma ya msihaya, nyimbo hii ilikua inaihamasisha jamii na imefumbwa tafauti na nyimbo zinazoimbwa sasa, nyimbo za siku hizi hazifumbwi, watu hujiimbua tu. Kwa mfano

Baba Amani usijibu tutajibu kina mama

Uyo kiongozi wao na bi Kipini kafanana

Sidiria hafu twaazimana japo kuwa langu pana

4.3.3 Ajira kwa Vijana

Kuwapo kwa nyimbo, wakati wa kampeni za uchaguzi, kunatoa ajira kwa vijana. Waimbaji, na waitikiaji wa nyimbo hizo, wengi wao ni vijana. Vijana hupewa ajira. Wakati mwingine, hupewa ajira ya muda, na wakati mwingine hupewa ajira ya kudumu. Waimbaji hutakiwa kufanya mazoezi ya muda mrefu, ili waweze kutimiza lengo la nyimbo hizo za kampeni. Vijana hao, hutumiwa kama ni vivutio vya uhamasishaji wakati wa kampeni hizo.

Akifafanua mmoja wa wasanii vijana wa kikundi cha Jeshi la Kujenga Uchumi

(J K U), Makame Bambuti, alisema, mimi nilitoroka skuli, na kwaumri wangu ni kijana mdogo, mwenye umri wa miaka 15, nilipoanza kuajiriwa na kuimba, katika kikosi hichi, kama si kuimba, ninaimani nisingeliajiriwa. Wapo wenzangu wengi wanaranda bure. Kwa hivyo ninaipenda kazi yangu na ninaithamini kwa sababu, inanilisha, inanivisha na inanifanya niishi vizuri. Kwa kuwepo haja ya nyimbo hizo, kila kipindi, vikundi vingi vya vijana hujitokeza, na kujikusanya pamoja, wakaunda vikundi vya ngoma. Vikundi hivyo, wakati mwingine, hudhaminiwa na wanasiasa na kuwapa chochote, na wakati mwingine, vikundi hivyo, hujisimamisha vyenyewe na kujitegemea.

4.3.4 Kujenga Maadili

Maadili ni mwenendo mzuri au mbaya ambao mtu anauonesha katika jamii yake. Kila jamii huwa na maadili yake, mtu akifuata kikamilifu maadili hayo, huambia mtu huyo ana maadili mema. Maadili hayo hayaendi kinyume na mila na desturi ya jamii husika. Katika kazi nyingi za wataalamu wameangalia jinsi kazi za fasihi simulizi

ikiwemo nyimbo zinavyoweza kutumika kama chombo cha kuadilisha jamii au cha kuifanya jamii hiyo kwenda kinyume na maadili yake. Haji (1994), Sengo (2010) na Robert, katika kazi zao wameonesha maadili mema na kuyafafanua. Mulokozi (1996) amesema nyimbo hutoa maadili mema katika jamii hasa nyimbo za kubembelezea watoto. Katika kubembeleza watoto, hupatikana burudani inayomburudisha, na kumliwaza mtoto, lakini pia hupatikana mawaidha, nasaha, na maonyo kuhusu maisha. Nkwera (1998) kwa upande wake amesema kuwa nyimbo zote humhusu binadamu. Dhima yake ni kuifunza jamii maadili katika nyanja mbalimbali za maisha, kiitikadi, kidini, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Hivyo nyimbo nyingi huimbwa kwa lengo la kumfahamisha binadamu miiko ya kila pahala na namna ya kuepukana nayo. Aidha huburudisha baada ya machofu na huliwazisha ndani ya huzuni.

Nyimbo za kampeni ya uchaguzi hazitimizi lengo la miiko ya jamii ya kizanzibari katika nyanja mbalimbali kama vile: mila zetu, utamaduni wetu na silka zetu.

4.4 Kutafuta Mbinu za Kufanya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi ziwe

Zinaleta Umoja Badala ya Utengano Katika Jamii ya Wazanzibari

Watafitiwa sabini na wane (74) waliojaza dodoso katika maoni yao walisema, ili nyimbo za kampeni ziweze kuleta umoja na kuondoa utengano katika jamii, watungaji na waimbaji hawana budi kutunga na kuimba nyimbo zenye kukuza umoja na kudumisha amani miongoni mwa wanajamii. Waache kutunga na kuimba nyimbo zenye kujenga chuki na kuhamasisha vurugu.

Omar Khamis Makame mtafitiwa alipokuwa akizungumza na mtafiti alisema, mbinu bora ya kuzifanya nyimbo za kampeni zilete umoja badala ya utengano ni utashi wa

viongozi wa kisiasa. Viongozi wa kisiasa wakazichukia nyimbo zenye lugha na maudhui ya utengano wakazikemea na wakakataza zisiimbwe, badala yake ziimbwe zile nyimbo zenye kukuza uzalendo na kuimarisha umoja, vikundi vyote vitafuata maelekezo hayo. Vilevile aliendelea kusema, kuwe na chombo cha kuzihakiki nyimbo zote kabla ya kuimbwa. Chombo hicho kitazipembua nyimbo zinazofaa na zisizofaa kuimbwa katika kampeni za uchaguzi.

Bibi Jina Saleh, Fatma Ali Iddi na Mwanaidi Haroub watafitiwa, mawazo yao yanalingana na wanasema, itolewe elimu ya uraia, umuhimu wa demokrasia na umuhimu wa uchaguzi, madhara na taathira zake kwa jamii nzima. Elimu ya kutii sharia itolewe kwa jamii nzima ili kila mwanajamii ajuwe kutii sharia zilizowekwa, baadae kiundwe chombo cha kusimamia nyimbo zote na atakaekiuka sharia, hatua kali zichukuliwe dhidi yake.

4.5 Uchambuzi wa Maudhui ya Nyimbo za Kampeni

Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu maudhui ya nyimbo. Yaani mafundisho na ujumbe unaopatikana katika nyimbo hizo. Nyimbo nyingi huimbwa ili kuendana na muktadha wa eneo au tukio husika. Pia ujumbe unaopatikana huakisi shughuli husika. Kwa mfano nyimbo zinazoimbwa katika harusi hulenga kutoa funzo kwa wana harusi na hujikita zaidi katika ujumbe wa kimapenzi na maisha ya ndoa. Nyimbo zinazoimbwa katika kazi huhimiza watu kufanya kazi na ujumbe wake huwa ni kama chachu ya watu kuendelea kuwajibika. Mulokozi (1996), ameeleza kuwa maudhui ya nyimbo yamejikita katika kuonya, kufunza na kuarifu. Pia huburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kutia hamasa katika kazi na vitani na pia kuomboleza.

Mbunda (1996), amefafanua juu ya maudhui ya nyimbo na kueleza kuwa maudhui ya nyimbo yanaweza kuelezea dukuduku na makero mbalimbali yanayoipata jamii. Alifafanua kuwa kila jamii ilikuwa na itaendelea kuwa na aina zake za nyimbo katika kuelezea dukuduku zao au mambo yanayoipata jamii. Nyimbo huelimisha, huikosoa na kuirekebisha jamii inapokuwa inaelekea kuzama katika dimbwi la upotofu. Mtazamo wa wataalamu hawa waliopitiwa katika utafiti huu, unaonesha dhahiri kwamba maudhui katika nyimbo ndio kiungo kikuu. Hilo limejidhihirisha pale walipoonesha baadhi ya nyimbo ambazo ndani yake zimebeba maudhui yanayolenga katika kufunza, kuonya, kuhamasisha na kutukuza.

Wamitila (2000) amesema, maudhui ni masuala na mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Ni maana anayoivumbua msomaji asomapo kazi ya fasihi. Maudhui na dhamira ni dhanna muhimu sana katika uhakiki wa fasihi. Uchunguzi wowote wa maudhui lazima uchunguze fani kwa kuwa dhanna hizi zinategemeana sana.

Madumulla (2009), anatilia nguvu kuwa, maudhui ni mawazo/ujumbe ambao humfikia msomaji. Senkoro (2011) anakazia kwa kusema maudhui ya kazi ya fasihi hujumuisha mawazo na pengine mafunzo yanayopatikana kwenye kazi ya mtunzi/msanii. Hadhira hulengwa wayapate mawazo na mafunzo hayo. Mawazo na mafunzo hayo, hayazuki tu bali hutokana na kuhusishwa na hali halisi ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi, hali ziliopo katika mfumo mzima wa jamii inayohusika.

Maudhui ndicho kipengele muhimu sana ambacho msanii anakusudia kukiwakilisha kwa jamii yake ili iweze kujifunza, kujikosoa na kujirekebisha juu ya mambo

yanayowazunguka. Madumulla (2009) anaweka bayana kuwa dhamira ni sehemu tu ya maudhui.

Watafitiwa wengi waliotafitiwa, walikiri kuwa nyimbo za kampeni zina maudhui tafauti kwa jamii ya Wazanzibari. Miongoni mwa maudhui hayo ni pamoja na umoja wa jamii ya Wazanzibari, maadili, mila, utamaduni na migogoro.

4.5.1 Umoja wa Jamii ya Wazanzibari

Utamaduni wa Wazanzibari umejengwa kwa misingi ya kujali na kuheshimu utu wa mtu. Utamaduni huo huimarisha tabia za kipekee ambazo ni adimu kupatikana katika sehemu nyingi zijulikanazo ulimwenguni. Mfano kama kupendana baina ya mtu na mtu na kuthamini utu wa mtu. Ukarimu na huruma umejenga mfumo wa udugu na kuwafanya Wazanzibar kuwa na dasturi ya kipekee. Hali hiyo ilijitokeza katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa. “Unguja ni Njema atayakae na aje” ni kauli maarufu sana kwa wenyeji na wageni waipendayo Unguja.

Nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu wa Zanzibar ziliimarisha umoja na kuendeleza mila na dasturi za Wazanzibari. Ulipozuka mfumo wa uchaguzi wa vyama vingi 1992, umoja uliyokuwapo uligawika sehemu mbili kuu. Kila sehemu moja ilizitumia nyimbo hizo kuimarisha umoja na mapenzi miongoni mwao. Bi Khadija Ibrahim Dau (Bi Hawa) msanii maarufu wa Kikundi cha Mila na Utamaduni cha Zanzibar, alisema, nyimbo huwa zinamgusa sana wakati anapoimba. Lengo na madhumuni ya kuimba kwao huwa ni kuimarisha umoja na mshikamano na kuiburudisha jamii. Lakini baadhi ya wasikilizaji huzifahamu vibaya

na kuzitafsiri kinyume cha lengo la nyimbo hizo. Kwa mfano, kwa kushangaa wimbo ya “Wasohaya wanamji wao”, uliyoimbwa na kikundi cha East Africn melody cha Zanzibar, uliimbwa hata kabla ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1990, lakini ulipoingia mfumo wa vyama vingi 1992, watu wakautumia kubezana na kudharauliana. wimbo huo unasema:

Binaadamu waso haya wana mji wao

Hawana lililo baya kwa upande wao

Jambo wakikutendea nisawa sawa kwao

Waallahimasikini roho zao.

Wazuri sura jamali maumbile yao

Kumbe ni watu thakili tabia zao

Huchunguza na kusaili mambo ya wenzao

Yao huyaficha mbali vibindoni mwao

Kweli waso haya wanamji wao.

4.5.2 Maadili

Maadili ni mwenendo mzuri au mbaya ambao mtu anauonesha katika jamii yake.

Kila jamii huwa na maadili yake, mtu akifuata kikamilifu maadili hayo, huambia mtu huyo ana maadili mema. Maadili hayo hayaendi kinyume na mila na desturi ya jamii husika. Katika kazi nyingi za wataalamu wameangalia jinsi kazi za fasihi simulizi ikiwemo nyimbo zinavyoweza kutumika kama chombo cha kuadilisha jamii au cha kuifanya jamii hiyo kwenda kinyume na maadili yake. Haji (1994), Sengo (2010) na

Robert, katika kazi zao wameonesha maadili mema na kuyafafanua. Mulokozi (1996) amesema nyimbo hutoa maadili mema katika jamii hasa nyimbo za kubembelezea watoto. Katika kubembeleza watoto, hupatikana burudani inayomburudisha, na kumliwaza mtoto, lakini pia hupatikana mawaidha, nasaha, na maonyo kuhusu maisha. Nkwera (1998) kwa upande wake amesema kuwa nyimbo zote humhusu binadamu. Dhima yake ni kumfunza mtu na jamii maadili katika nyanja mbalimbali za maisha, kiitikadi, kidini, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Hivyo nyimbo nyingi huimbwa kwa lengo la kumfahamisha binadamu miiko ya kila pahala na namna ya kuepukana nayo. Aidha huburudisha baada ya machofu na huliwazisha ndani ya huzuni.

Nyimbo za kampeni ya uchaguzi hazitimizi lengo la miiko ya jamii ya kizanzibari katika nyanja mbalimbali kamavile:

4.5.3 Mila na Utamaduni

Adam (2014) ameeleza kwamba utamaduni ni mfumo au utaratibu wa maisha ambao jamii inaufuata katika maisha yake ya kila siku ikijumuisha mila, desturi, miiko, jando na unyago. Utamaduni wa jamii ndio hutoa dira na mwelekeo wa namna mambo mbalimbali katika jamii yanapaswa kuwa na kuendeshwa na wanajamii wote ili kuleta uhusiano mzuri miongoni mwa watu, upendo, amani, ushirikiano na kuheshimiana katika jamii.

Kimsingi, kila jamii ina utamaduni wake kulingana na mazingira ya jamii husika kisiasa, kijamii, na kadhalika. Zanzibar ina mitindo yake maalumu ya mavazi kwa watu wake ikiwa ni sehemu ya utamaduni wake. Mitindo hiyo, huonesha dasturi na

ustaarabu wa watu wa Zanzibar. Mavazi hayo hujali zaidi kujisitiri, kama Uislamu unavyotaka. Kwa muda mrefu, maadili hayo katika mavazi kwa Wazanzibari yaliendelezwa kurithishwa, kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa sasa, hali hiyo ni tafauti. Zanzibar kumebadilika hasa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, kumezidi kumomonyoka kimaadili, kwa kuvaa na kucheza kinyume na dasturi za wasichana. Haya yameelezwa na watafitiwa wengi akiwemo bwana Khatibu Haji Mchenga, mhojiwa, bwana Bakari Makame Bakari(Gunya) ambae ni mmoja wa wahojiwa na bibi Hidaya Khamis ambae pia ni muhojiwa walisema kuwa, mmomonyoko wa maadili umechangiwa na kuwapo kwa uhuru usio na mipaka, wakati wa kampeni za uchaguzi.

Hivi sasa, mavazi yanayovaliwa na vijana wengi wa kike ni yale yasiyojali heshima wala stara. Mavazi hayo huwa ni mafupi na yenye kubana sana mwilini. Kwa jumla, mavazi hayo yametawaliwa na mvuto wa kufurahisha watu katika kampeni. Kwa kuthibitisha hali hiyo, wengi wa watafitiwa, waliofanya mahojiano na mtafiti, walikiri kuwapo kwa hali hiyo wakati wa kampeni, na sasa hali hiyo imeanza kuzoeleka katika jamii.

Mwalimu Ibrahim Mohd Habibu, mmoja wa wahojiwa, katika skuli ya Sekondari ya Lumumba, aliongezea kusema kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili wakati wa kampeni za uchaguzi. Vijana hasa wa kike huvaa mavazi yaliyo kinyume na utamaduni wa kizanzibari. Nyimbo zinazoimbwa wakati wa kampeni, pia zinaharibu mila na dasturi ya Wazanzibari katika lugha. Watu hutumia lugha za matusi bila kujali wala aibu. Nyimbo zinainbwa kiholela, hazipitiwi wala hazikaguliwi na

taasisi zinazohusika, huimbwa matusi bila ya kujali zinaimbwa wapi na wakati gani, na hakuna mtu ambaye anazikataza. Mwalimu Ibrahimu alifafanua zaidi tafauti ya maneno ya nyimbo na mavazi ya leo na ya zamani. Alisema, wasanii wa zamani walijenga haiba kwa kuvaa na kutumia maneno yenye usanii wa hali ya juu na kuvaa mavazi yenye heshima kubwa. Bw. Bakari Makame Bakari (Gunya) alisema, kwa masikitiko. Jamii yetu ya leo imekuwa kama watoto wa mbuzi, waliokosa mchungaji. Inasikitisha kuona watoto wetu wanapelekwa viwanjani uchi. Wanachezeshwa uchi. Wanaimbushwa matusi mbele ya macho yetu. Hii ni dunia gani? Tunakwenda wapi? Kwanini sisi hatukulelewa hivyo wakati ule? Kimezidi nini leo? Huyu katukana na yule kajibu matusi, utamaduni huu tumeupata wapi? Akitoa mfano wa nyimbo za zamani aliimba :

Watoto mnara, huo heria we Unguja

Watoto mnara, huo heria we Unguja

Ushafaulu rasi tieni nanga, maji maranga.

Huu ni wimbo uliyoimbwa na kikundi cha ngoma ya asili ya Mdema ambacho kwa sasa hakipo tena, lakini wimbo huu bado huimbwa na viongozi ukijenga umoja na ushirikiano, hauna matusi wala kejeli. Nyimbo za leo ni matusi na kejeli, mathalani wimbo wa Fisadi Kiwembe ulioimbwa na East African Melody kama ufuatavyo;

Jamani mnamjuwa huyo fisadi kiwembe au mnamsikia tu,

Naam tunamjuwa huyo fisadi kiwembe mgombanishaji watu,

Mgombanishi femili, mfitini majirani msambaratisha pembe,

Yumo miongoni mwetu roho yake ina kutu,

Tatizo lake hapendi maendeleo ya mtu,
Fisadi kiwembe ana roho mbaya,
Ewe fisadi kiwembe hebu acha laana zako,
Kazi unayoijuwa kugombanisha wenzako,
Bibi wewe ni mbeya uongo ndio sera zako,
Kila nyumba waingia kuanzisha chokochoko,
Pia unakuwadia mabwana wa shoga zako,
Na kuvunja zao ndoa kwa choyo na wivu wako.

Kila jamii ina maadili yake ambayo hujengwa kwa kutumia nyenzo mbalimbali. Nyimbo ni moja kati ya nyenzo za kujengea maadili katika jamii. Nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu Zanzibar zina changia kuporomoshia maadili, kwa kuchochea vitendo vya uasharati.

Jamii ya Wazanzibari, kwa kiasi kikubwa, ni yenyekufuata imani ya Kiisilamu, imani hii inawazuwia vijana, hasa wanawake kuranda ovyo ovyo. Kawaida vijana wa kike wa Kizanzibari huwapo nyumbani kwa muda wote isipokuwa hutoka kwa dharura maalumu. Kampeni za uchaguzi na hasa zinapoambatana na ngoma zenye nyimbo, huwafanya vijana hao kutoka majumbani mwao kwa wingi.

Vijana hao wanapokuwa huko nje huwa huru kufanya vitendo vyovyote ambavyo viko nje ya maadili na silka za Wazanzibari. Kwa kutumia hojaji, majadiliano na uchambuzi wa maandishi ilibainika kwamba, nyimbo za kampeni za uchaguzi, wakati wa kampeni zinachangia kwa kiasi kikubwa vitendo vya uharibifu wa tabia.

Watafitiwa wengi walieleza jinsi uasharati unavyofanywa hadharani. Bi Daulat Adalla Said, Mkuu wa Idara ya Kiswahili kwa Wageni, Chuo Kikuu Cha Taifa (SUZA), akizungumza na mtafiti, alisema, “mtu mwenye haya zake, hawezi kwenda kwenye kampeni kwa kuwa wapigaji wa ngoma ,waimbaji, wachezaji, wote hawana haya, kwa vitendo wanavyovifanya, ni kinyume kwa mila zetu, kinyume na desturi zetu, kinyume na imani zetu.Vijana kucheza uchi, kuvaa nguo zisizo na heshima. Matokeo ya yote hayo ni kufanya vitendo vya uasharati”.

4.5.4 Migogoro

Mlokozi (1996) alifafanua kwa kusema migogoro ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi za fasihi. Migogoro inaweza kuwa kati ya wahusika, familia zao, matabaka yao, au hata katika nyadhifa mbalimbali. Vilevile Wamitila (2006) amesema migogoro yaweza kuwa ya kiuchumi, kijamii, migogoro ya nafsi, na migogoro ya kisiasa ambayo hujitokeza katika mitazamo tofauti kulingana na mtiririko wa visa, beti na matukio yanavyopangwa na mwandishi. Saluhiya (2012) amesema migogoro ni mivutano au mikinzano inayojitokeza katika kazi za fasihi. Mgogoro unaweza kutokea au kukuzwa na uhusiano uliopo kati ya mawazo mbalimbali na matendo mbalimbali. Mgogoro unaweza kuwa baina ya wahusika wawili, kati ya mhusika na mazingira au kati ya wazo na wazo. Mara nyingi migogoro katika kazi ya fasihi inaweza kuwa ya kiuchumi, kiutamaduniwa binafsi na mgogoro wa kisiasa.

Watafitiwa wengi akiwemo bibi Daulat Abdalla Said, bibi Latifa Khamis Mohammed, bibi Mwanahawa Mohammed, bwana Said Moh'd na mwalimu Masoud Yakoub walisema, nyimbo za kampeni zinapoimbwa huchangia sana chuki,

uhasama na ugonvi miongoni mwa wanajamii. Bibi Mwanahawa akitoa mfano alisema, wimbo wa Wasohaya wanamji wao, wimbo huu ulipoimbwa ulizusha chuki na uhasama miongoni mwa wanajamii. Majirani walinuniana, wakakosa kusemeshana kwa sababu mmoja anatoka Unguja na mwingine anatoka Pemba . Wa Unguja husema wa Pemba ndiye asohaya, na wa Pemba husema wa Unguja ndie asohaya.

Pia hojaji zilizo jazwa na watafitiwa wapatao 78 wengi wao walikiri kuwepo kwa chuki, uhasama na ugomvi kwa kipindi chote cha kampeni za uchaguzi na wengine huendeleza hata baada ya kampeni. Tukiangalia kwa undani zaidi, kila kundi la watafitiwa kupitia sampuli yao lilikiri kushuhudia hali ya migogoro katika jamii wakati wa kampeni unaosababishwa na nyimbo zinazoimbwa kwa mfano, vijana walisema kuwa hali ya ugonvi hutokea pale wanaporushiana maneno ya vijembe yaliyokuwemo ndani ya nyimbo zinazo imbwa, wakikutana njiani wakiwa wanarudi au wanakwenda kwenye mikutano.

Kwa upande wa waandishi wa habari waliojaza hojaji, wengi wao walisema kuwa, wao ni mashuhuda wa kubwa wa kushuhudia migogoro mingi inayotokea katika jamii inayosababishwa na nyimbo za kampeni. Watu hufika kupigana na kutiana vilema vya maisha kutokna na hamasa wanazozipata kutokana na nyimbo za kampeni. Hayo hutokea viwanjani , mitaani na sehemu nyengine zinazowakutanisha watu wenye mitazamo tafauti ya siasa.

Wasanii wa taarab wakiwa ni wadau wakubwa wa sanaa ya nyimbo za kampeni walikiri kuwepo kwa migogoro mingi katika jamii inayosababishwa na nyimbo

hizo. Bibi Fatma Juma msanii wa kikundi cha mila na utamaduni cha Zanzibar, alipokuwa akihojiana na mtafiti alisema, wakati mwengine unatunga nyimbo ya kupasha kwa makusudi lakini wakati mwengine nyimbo hutafsiriwa vibaya kutokana na wakati na mazingira ya uimbaji wa nyimbo hiyo. Kuzomeana na kubezana wakati wa uimbaji na kuitana majina yasiyofaa huchangia sana migogoro inayoibuka wakati wa kampeni kupitia nyimbo zinazoimbwa wakati huo.

Kwa mfano wimbo wa Fisadi Kiwembe unasema

Jamani mnamjuwa huyo fisadi kiwembe au mnamsikia tu

Naam tunamjuwa huyo fisadi kiwembe mgombanishaji watu

Mgombanishi femili, mfitini majirani msambaratisha pembe

Yumo miongoni mwetu roho yake ina kutu

Tatizo lake hapendi maendeleo ya mtu

Fisadi kiwembe ana roho mbaya kama chatu

Ewe fisadi kiwembe hebu acha laana zako

Kazi unayoijuwa kugombanisha wenzako

Mtu wewe ni mbeya uongo ndo sera zako

Kila nyumba waingia kuanzisha chokochoko

Wimbo huu ni wa kashifa. Mtu kuitwa fisadi tena fisadi kiwembe. Kiwembe ni kifaa kidogo lakini kina kashifa kubwa. Mtu anayeimbwa hapa hukosa amani, hukosa furaha, huwa ni mwanzo wa uhasama na mgogoro usiomalizika. Mawazo kama hayo yamejitokeza kwa wasomi wengi kupitia dodoso walizozijaza. Wengi wao

wamethibitisha kuwa migogoro mingi ilisababishwa na jazba inayotokana na nyimbo za kampeni, walieleza kuwa nyimbo za kampeni hutumia maneno ya kejeli, mipasho, mafumbo, kashfa na vijembe, mambo haya ndiyo yanayopandisha mori kwa wengine na kushindwa kustahamili na kupelekea kutokea kwa migogoro mingi katika jamii.

Bwana Rai wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar wakati alipozungumza na mtafiti alisema, migogo inayosababishwa na nyimbo za kampeni za uchaguzi wakati wa kampeni, ni vigumu kumalizika ikiwa jamii haijajitambua. Kwanza kuwekwe kanuni maalumu za kampeni zitakazopelekea watu kufanya kampeni kwa kufuata taratibu za kuheshimiana na kutumia ustaarabu wa kuvumiliana kimila na kidasturi za Kizanzibari. Pili kuwe na Taasisi maalumu ya ukaguzi wa kazi zote za sanaa ili kulinda maadili na kukuza uzalendo.

Watafitiwa wengi walikubaliana na mawazo hayo walipokuwa wakijibu swali lililohoji, mbinu gani zitumike ili nyimbo za kampeni zilete umoja badala ya utengano.

4.6 Hitimishi

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu. Uwasilishaji na uchamuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia lengo la utafiti na umeongozwa na mkabala wa kiidadi na usio wa kidadi. Vili vile sura hii imefafanua michango ya nyimbo za kampeni na dhamira zinazopatikana katika nyimbo hizo. katika sura inayofuata, tutatoa muhtasari, hitimishi, matokeo ya utafiti na mapendekezo kwa ajili ya utafiti wa baadae.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ametoa hitimishi la kazi hii kwa kueleza utaratibu mzima uliofuatwa. Sura hii imegawika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza, imeeleza muhtasari wa utafiti mzima. Sehemu ya pili, inatoa matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sehemu ya tatu, inaeleza mchango wa utafiti. Sehemu ya nne inaeleza mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kuhusu maudhui ya nyimbo za kampeni, na sehemu ya mwisho inapendekeza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2 Muhutajari wa Tasnifu

Utafiti huu uliochunguza Maudhui ya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi Mkuu Zanzibar, ulifanyika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini, Magharibi Unguja. Jumla ya watafitiwa 85 walishiriki katika utafiti huu, wakiwemo, wasanii wa nyimbo za kampeni, vijana, watu wazima, walimu wa Skuli za Wilaya ya Mjini zikiwemo Lumumba, Hamamni, Vikokotono, Mwembeladu na Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA). Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya maskanini, maktabani, usaili, hojaji na kutumia vyombo vya kidijitali. Vile vile data zimechanganuliwa kwa mkabala wa kiidadi na usio wa kiidadi. Mpangilio mzima wa kazi hii ulikuwa kama ufuatavyo:

Sura ya kwanza, imeanza utangulizi wa jumla wa mada ya utafiti. Ikifuatiwa na usuli wa mada kwa kuelezea maana ya nyimbo, pia mtafiti alizungumzia tatizo, sababu za mivutano katika vipindi tafauti vya historia ya kampeni za chaguzi kuu Zanzibar,

lengo la utafiti, madhumuni maalumu, maswali ya utafiti, matatizo yaliyojitokeza katika utafiti, na eneo la utafiti huu.

Sura ya pili, ilifafanua kazi tafauti za watangulizi zikiwemo, vitabu, majarida, mitandao na utafiti ambao kwa kiasi kikubwa umetoa maelezo yanayopatana na mada iliyotafitiwa. Kutokana na hayo, mtafiti alibaini kuwa, si waandishi wengi, waliozungumzia Nyimbo za Kampeni ya Uchaguzi Mkuu Zanzibar.

Sura ya tatu inazungumzia namna utafiti ulivyofanyika. Mbinu mbalimbali kama vile mpangilio wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo lililotumika kwenye utafiti, jumla ya watafitiwa, sampuli iliyotumika na namna ilivyopatikana, ukusanyaji wa data na vifaa vilivyotumiwa katika kukusanyia data.

Sura ya nne imeonesha namna data zilivyokusanywa na kutafsiriwa. Data hizo zilichambuliwa, kwa kutumia uchambuzi wa kifafanuzi. Sura ya tano mtafiti ametoa hitimishi la kazi hii kwa kueleza utaratibu mzima uliofuatwa. Sehemu hii ina vipengele vifuatavyo: Muhutasari wa tasnifu ambao umebeba mambo machache yaliyojitokeza katika kila sura, matokeo yaliyopatikana katika utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa, na mwisho mapendekezo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Katika kuandika tasnifu hii, lengo lililoongoza lilikuwa ni kuchunguza maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu katika jamii ya watu wa Zanzibar kuanzia mwaka 2000 hadi 2010 na hatimae kudhihirisha na kuwasilisha kwa jamii ya

Wazanzibari matokeo yenye suluhu za kuleta amani, usawa na umoja miongoni mwa wanajamii kutokana na lengo hili, mtafiti aligundua kuwa, nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu, Zanzibar, zina maudhui na majukumu mengi ndani ya jamii ya Wazanzibari, kama ilivyobainishwa na watafitiwa. Maudhui na majukumu hayo ni :

Kuporomoka kwa maadili ya vijana wa Zanzibar, kuliongezeka kila uchao, kutokwa na haya na kufanya vitendo vya uasharati imeanza kuwa ni tabia, vile vile, mabadiliko na mienendo isiyoridhisha kwa vijana imeanza kuwa ni tabia kwa sababu ya kuiga vitendo wanavyoviona na kuvisikia. Pia Fasihi inavizwa, inapunguzwa ladha yake kwa kusemwa wazi wazi kila kitu.

Utafiti huu umebaini kuwa nyimbo za kampeni zinaleta umoja na mashirikiano miongoni mwa Wazanzibari. Zinajenga uhusiano mzuri na zinaleta mshikamano ndani ya jamii. Zinajenga hamasa na uzalendo, Wasanii wengi walisisitiza hivyo.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na matokeo na utafiti huu, yametolewa mapendekezo yafuatayo: nyimbo zote za kampeni zipitiwe na bodi ya sensa ya nyimbo kabla ya kuimbwa. Taasisi hiyo ifanye kazi kwa karibu sana na kwa pamoja na watunzi wote wa nyimbo za kampeni kwa lengo la kudhibiti kuharibiwa sanaa hiyo.

Vilevile tunapendekeza utafiti zaidi ufanyike katika kulinganisha na kutafautisha tija ya nyimbo za kampeni na hasara zake wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu Zanzibar kwa faida ya Wazanzibari wa leo na wajao.

5.5 Mapendekezo Juu ya Utafiti Fuatishi

Utafiti huu umechunguza maudhui ya nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu Zanzibar. Kutokana na lengo la utafiti huu, na kukosekana kwa watafiti wengi waliofanya utafiti kuhusu nyimbo za kampeni, kuna haja kubwa kwa watafiti wajao, kutafiti athari za nyimbo hizo, kwa wasanii.

Vile vile, ninapendekeza utafiti zaidi ufanyike katika kulinganisha na kutafautisha tija ya nyimbo za kampeni ya uchaguzi mkuu, Zanzibar na hasara inayopatikana wakati wa kampeni hizo kwa maendeleo ya jamii ya Wazanzibari.

MAREJELEO

- Abdalla, B. A. (2011). *Athari za Mabadiliko katika Nyimbo za Taarab: Lugha na Uwasilishaji*. Tasnifu ya M.A. Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.
- Abeid, K. A. (1973). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Adam, O. A. (2014). *kuchunguza dhamira za kijamiina kiutamaduni katika riwaya ya Kiswahili mfano kutoka Kuli na Vuta N’kuvute*, Tasnifu ya PH.D Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam, Tanzania.
- Ameir, D. (1983). *Fasihi Simulizi Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House
- Andrews, R. (1993). *Research Questions*. London: The Tour building 11 York Road
- Badru, H. (2012). *Matumizi ya Taswira Katika Nyimbo za Taarab*. Tasnifu ya uzamili chuo kikuu Dodoma, Tanzania.
- Baraza la Kiswahii la Zanzibar, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University press.
- Child.D. (2004). *Psychology and the Teacher*. New Delhi: Midas Printing International Ltd
- Daud, A. (2012). *Maudhui ya Nyimbo za Daku*.Tasnifu Chuo Kikuu Cha Dodoma. Tanzania.
- Enon, B. (1998). *Education Research, Statistcal and Measurement*. Kampala: Makerere University,
- Finnegan, V. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press.

- Gora, H. A. (2011).” Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo”. Tasnifu Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) Zanzibar, Tanzania.
- Haji, H. G. (1994). *Kimbunga: Tungo za Visiwani*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar-es-Salaam
- Hamadi, S. O. (2005). Athari za nyimbo za kizazi kipya kwa jamii ya Zanzibar”.Tasnifu ya B.A (Ed) SUZA. Zanzibar, Tanzania.
- James, J. na Faustino, M. (2011). *Kiswahili Kidato cha Tano*, Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, Method and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Limited.
- Maalim, T. na Birch. A. (1998). *Introductory Psychology*. New York: Palgrave Fifth Avenue
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printers Stationary.
- Mayoka, J. K. (1993). *Mgogoro wa ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salam: Ndanda Mission Press.
- Mbogo, E. (2015). *Sadaka ya John Okelo*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Mdungu, A. (2007). *Arudhi ya Ushairi wa Kiswahili*. Zanzibar: Al-mafazy.
- Mdungu, A. (2000). *Malenga wa uswahilini*. Zanzibar: Al-mafazy.
- Mzee, A. F. (2011). “Athari za Nyimbo za Taarabu ya Mipasho kwa Jamii ya Wazanzibari”, Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. Tanzania.
- Mohamed, M. S. (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press:
- Msokile, M. (1972). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi EAEP.

- Mulokozi, M.M. (2006). *Fasihi ya Kiswahili-OSW105*, Chuo Kikuu Huriacha Tanzania.
- Mulokozi, M.M (1996), *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*, TUKI. Dar es salam
- Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mapuri, O. R. (1996). *The 1964 Revolution: Achievements and Prospects*. Dar es Salaam: Tema Publishers Company Ltd.
- Nasser. I. I. (1999). *Kinyang'anyiro na Utumwa*, Oman: Ruwi Sultanate of Oman.
- Nkwera, F. M. V. (1998). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyu*, Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Omary, M. (2011). "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi," Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Tanzania.
- Odeo, I.I na Geoffey, M. (2008). *Fani ya Isimu Jamii*. Nairobi: Oxford University Press.
- Opie, C. (2010). *Doing Educational Research*. London: SAGE Publication Inc.
- Patrick, J. M. (2003). *Action Research*. London: The Tour building 11 York Road.
- Robert, S. (1991). *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Dar es Salaam: Printpark (T) Ltd.
- Said, (2005). "Maudhui ya Nyimbo za Watoto" Tasnifu Chuo Kikuu Cha Dar es Salam. Tanzania.
- Salum, O. M. (2010). "Mchango wa Nyimbo za Unyago Katika Kumkomaza Mwari Kiunyumba Wilaya ya Kinondoni" Tasnifu Chuo Kikuu cha Kiislamu. Kampala Uganda.

- Santrock, W. J. (2003). *Psychology*, New York: McGRAW-Hill Company.
- Saluhaya, M.C. na Suleiman, M. A. (2012). *Nadharia na Tahakiki ya fasihi*. Dar es Salam: S T S Publishers.
- Seif, G. D. (2011). “Nyimbo za Jando na Unyago Katika Jamii ya Kikaguru” (tasnifu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.
- Sengo, S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: Akademiya/ AERA Kiswahili Researced Products
- Sengo, S. Y. M. (2010). *Diwani ya Midulu*. Dar es Salaam: Akademiya/ AERA Kiswahili Researced Products
- Senkoro, F. E. M. K. (1984). *Fasihi*, Dar es Salaam: Dar-es-salam Publicity Centre.
- Sheriff, A. (1991). *Zanzibar Under Colonial Rule*. New York: Ohio University Press.
- Sheriff, A. (ed.) (1995). *The History and Conseration of Zanzibar StoneTown*. London: James Curry Publishers.
- Serekali ya Mapinduzi Zanzibar, (2014). *Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kuanzia mwaka 1964 hadi 2014*, Idara ya habari maelezo, Zanzibar.
- Simai, H. A. (2005). “Mafunzo Yanayopatikana Katika Nyimbo za Harusi Katika Ndowa za Unguja”, Tasnifu. Chuo Kikuu cha Taifa SUZA. Zanzibar, Tanzania
- Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Nairobi: Serengeti Bookshoop.
- Suleiman, S. M. (2009). “Mafunzo ya Utetezi na Ushawishi”. Haijchapishwa. Zanzibar, Tanzania.
- Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. (1983). “Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili iii-Fasihi” Dar es Salam. Tanzania.

- Taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni Zanzibar, (1983). *Fasihi Simulizi*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Taasisi ya Kiswahili na Lugha za kigeni Zanzibar, (1992). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988). *Kiswahili Sekondari*. Da es Salaam: Kitabu Commercial Ltd
- TAKILUKI. (1982). *Hapa na Pale: Tungo za Sanaa*. Zanzibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Welling, J. (2000). *Educational Research*. London: The Tour building 11 York Road.
- Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa fasihi. Misingi na Vipengele vyake*, Nairobi: Foenix Publisher ltd.
- Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*, Nairobi: Phoenix Publisher Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi. Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.
- Wavula, R. M. na Njogu, K. (2001). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai industries Ltd.

VIAMBATANISHI

Kiambatanishi 1: Nyimbo za Kampeni

Hizi ni nyimbo zilizoimbwa na kikundi cha mila na utamaduni cha Zanzibar

1 UCHAGUZI

Ushaguzi umefika	Sote tukachagueni
Tusifanyeni dhihaka	tukabaki majumbani
Tena tufanye haraka	haki yetu tujuweni
Tena tufante haraka	haki yetu tujuweni
Haki yetu kuchaguwa	yule tunaye mtaka
Bila ya kuhadaiwa	wala kuwekwa mipaka
Au rushwa kuchukuwa	hapo tutadhalilika
Au rushwa kuchukuwa	hapo tutadhalilika
Tuchague anofaa	kazi kuja tufanyia
Sio aliye zowea	rushwa kujipokelea
Au anye hadaa	mali ujikumbizia
Au anye hadaa	mali ujikumbizia
Tushikaneni mikono	kwa mapenzi kuchagua
Kisha tuleni vinono	pamoja kufurahia

Tusije tafuna meno	matokeo kuchukia
Tusije tafuna meno	matokeo kuchukia
Sote tukachagueni	amani hazinab yetu
Umoja tuushikeni	chuki si tabia yetu

2 MOLA IBARIKI NCHI YETU

Mola wetu ya manani ibariki nchi yetu

Izidi kuwa amni	tukuze uchumi wetu
-----------------	--------------------

Amani kitu muhimu	hili tunalitambua
-------------------	-------------------

Hata kwa mwenda wazimu	amani huhitajia
------------------------	-----------------

Seuze watu adhimu	akili zilotulia
-------------------	-----------------

Seuze watu adhimu	akili zilotulia
-------------------	-----------------

Amani kwa wanadini	huabudu kwa utuo
--------------------	------------------

Padiri na makuhani	huhubiri kwa matao
--------------------	--------------------

Shekhe na wanavyuoni	hutulia na ya kwao
----------------------	--------------------

Shekhe na wanavyuoni	hutulia na ya kwao
----------------------	--------------------

Amani kwa wakulima	hulima kwa kutulia
--------------------	--------------------

Hawalimi na kuhama	mazao kuyakimbia
--------------------	------------------

Huvuna tena kilima	kila siku ikingia
--------------------	-------------------

Huvuna tena kilima	kila siku ikingia
--------------------	-------------------

Amani ikipotea	kuitafuta ni taabu
----------------	--------------------

Hata kule kusinzia	kwa mtu huwa ajabu
Balaa itaingia	amani yetu dhahabu
Balaa itaingia	amani yetu dhahabu

3. RABI TWAOMBA SALAMA

Rabi tunaomba kwako	shufaakutuingia
Nidhaifu waja wako	maramoja kukosea
Aula hula makoko	haraka ikiwangia
Husahau waendako	wakapotewa na njia
Hucheza bila kujua	wacheza mchezo gani
Mdundo ukiwangia	mara hungia porini
Kisha husahau njia	hubakia situni
Huwa wamesha potea	hawarudi abadani
Wapigaji huchochea	lele kuwatamkia
Vibogoyo nao pia	mbuyu hujitafunia
Na viwete hutambaa	kwenda wasikokujua
Yaleli nyingi hupaa	kuwavuta wasojua
Mola tuoneshe njia	kwetu iliyosahihi
Uchaguzi unongia	wote uwe wa halali
Porini tusije ngia	tukala tusicho wahi
Bilisi walo pania	wapeperushe kwa hili
Uchaguzi nchi yetu	amani twajiombea

Kampeni uwanjani ziwe zenye kutulia

4. DEMOKRASIA

Demokrasi si chuki wenyewe kuchukiana

Na wala si unafiki uongo kuambizana

Lakini ni urafiki wenyewe kupongezana

Lakini ni urafiki wenyewe kupongezana

Demokrasi si ngumi wenyewetu kupigana

Na wala sio umimi wenyewe kuoneshana

Si alimu si msomi kiburi kufanyiana

Si alimu si msomi kiburi kufanyiana

Demokrasi ni zamu wenyewe kupangiana

Kwa kipindi maalumu wadhifa kushikizana

Huyu tukimtuhumu tujuwe vya kumbana

Huyu tukimtuhumu tujuwe vya kumbana

Demokrasi furaha watu kufurahishana

Kusema bila karaha watu wakatambuana

Pia kwenda kwa madaha popote unapona

Pia kwenda kwa madaha popote unapona

Demokrasi eeee demokrasi sighera wala hiana

Demokrasi eeee demokrasi si chuki fitina.

5. AMANI

Amani amani amamani	tuihamini amani
Tanzania tulongayo	tuihubiri amani
Tunapokwenda kondeni	tuihubiri amani
Baraza la wawakilishi	tuihubiri amani
Tunaopkwenda majimboni	tuihubiri amani
Tukenda misikitini	tuihubiri amani
Tukenda makanisani	tuihubiri amani
Tunapokwena shulei	tuihubiri amani
Nchi yetu ya sifika	kwahapa ulimwenguni
Amani tuloiweka	wengi waitamani
Tuithamini kihakika	tusiufanye utani
Ikija ikitoweka	hairudi asilani
Amani amani	tuihamini amani
Ukabila na udini	nihatari duniani
Tukae kwa umakini	usiingie nchini

Nchi zimeangamia	hazikukaa makini
Ukabila kuingia	sasa ziko hatarini
Amani amani	tuithamini amani
Nchi nyingi Afrika	zimeingia vitani
Wananchi wateseka	imekuwa tafrani
Kucha wanahangaika	hawajuwi wafanyani
Nchi wameziona doka	nawao hawazikani
Uchumi umeanguka	hali zimekuwa duni
Imengia patashika	maadui wamo ndani
Tanzania tunataka	tusingie mtegeno

Chanzo Issa khamis Issa wa Kikundi cha Mila na Utamaduni

Hizi ni nyimbo zilizoimbwa na kikundi cha Sanaa Mkoa Mjini Magharibi

6. MAMA KIKWETE

Mama kikwete karibu

Mola akupe Baraka

Hapa na unakotoka

Sote twajua wajibu

Twangoja siku ikifika tutatoa pigo la mwaka.

Rabi dua ziitikie ashinde baba kikwete

Kiumbe aso makeke mcheshi tabia yake hutumikia yoyote

Zipo nyingi sifa zake Kikwete twa zitambua

Heri tujaalie manani ashinde baba

Amani kura zote visiwani

Uzalendo kaweka usoni

Habgui kwao nani

Alicho fanya kibuteni micheweni mkoani kafanya

Kina mama kina baba vijana tumeshikana

Kurumbizi hatutishi, wabunge diwani wakilishi

Tutazijaza zao pishi baba Amani baba Kikwete

Wanakazi bila wasi wasi.

Chama pinduzi mlezi sera zake

Ziko wazi hazipendi ubaguzi

Wakulima na wakwezi

Wengi wamepanda ngazi

Baada ya mapinduzi.

7. NAANGURUME

1. Naangurume Komando

Naa ngurume

Wametusaliti kwa mapanga

na mawe

Msitu wa Simba haulali

nguruwe

- | | | |
|----|---------------------|--------------------------|
| 2. | Komandoo uburudi | fanya kazi bila wasi |
| | Wameanza na esidi | sasa mpaka vinyesi |
| | Amaa lisilobudi | umarua sasa basi |
| 3. | Komandoo usokedi | twakufurahia hadi |
| | Hotuba yako ya Iddi | Kichwani tumerikodi |
| | CCM tubaridi | kwa sheria ni waledi sie |
| | Naangurume Komando | Naa ngurume |
| | Naangurume Komando | Naa ngurume |

8. BABA BILALI

Sasee sase we Mwam bughudhi Bilali
 Kwa sababu hana Sase huo ubaya
 Kina mama ee kina mama ee
 Twa vaa Vitenge na mitandio na kanga njema

Kurejea kaniki huo muhali tunasema
 Majina ni Sabrina na dada Amina
 Si Mjakazi na mtwana

Baba Bilali ee, baba Bilali shika usukani
 Jahazi lako lisende mrama
 Kina mama tutayari Baba Bilali lolotesema

Si kwangumi, Si kwa teke Si bunduki piaa

Tuimara tumesimama jamani sase

Kina mamaee Kina mama ee

Mkoa wa Mjini tumefurahika Leo si haba

Kuchaguliwa kwako kinamama hatuna shida

Tunacheza kila fani twajiringia

Mwatuona kila mmoja jamani sase

Kiitikio : SaseSasee sase we Mwam bughudhi Bilali

Kwa sababu hana Sase huo ubaya

9. WAKAANGA MBUYU

Wakaanga mbuyu Wajibu kulaaniwa

Wasababisha Nyumba za enzao kubomolewa

Wakunje na milioni zao wanatumia

Natuchekecheni Vibaya kutumiliwa

Wengine makuhani watu wabaya watugawa Visiwani

Pemba na Unguja Sote ni kitu kimoja

Pole baba Komando Polea wajibu tunaujuwa

Kwa kila Mtanzania kulinda yetu Amani

Baya lisijetokea likaondoa murua

Usijione mnyonge hapa ni petu nyumbani ee

Maneno yote yaronge tutakamata kwa yakini

Fimbo kura uzichonge tuwachape wapinzani

Baba Komando murua Sisi hatutopanguaee

Tuko radhi tumeamua Uongozi huna doa

Hupendi kutubagua kuna mama tunaelewa

Kina mama zetu haki zimo mwetu mikononi

Wengine wapanda Vyombo wengine tumiradini

Wengine ni mawaziri tazamani maidarani

Chanzo :bi Kipini wa kikundi cha sanaa Mkoa Mjini Magharibi

Hizi ni nyimbo zilizoimbwa na kikundi cha sanaa cha Imarisha

9. HAMWISHI KUZUA

1. Mara hili wee mara lilie haweshi kuzua

Mara hili wee Mara lile Wameshazowea

Mashule wameyachoma

Maghala wameyachoma

Na jaana wameripua

- | | | |
|----|---------------------------------------|----------------------|
| 2. | Yakarume yarudi | Anae choma huchomwa |
| | Naiba sio utani | wapewe kweli adhabu |
| | Kali hawa makuhani | nchi wataiharibu |
| | | |
| 3. | Si watu wenye imani | hawa wasihurumiwe |
| | wawe jela maishani | hata wapae ja mwewe |
| | Wakati umeshafika | naitumike sheria |
| | | |
| 4. | Jaji asowajibika | haraka kuondolewa |
| | Haraka kuoneolewa | wakachunge Ngombe |
| | Mjini kuondolewa | hao kwetu ni wazembe |
| | Mara hili wee mara liliehaweshi kuzua | |
| | Mara hili wee Mara lile | Wameshazowea |

11. BALAHAU

- | | | |
|----|-------------------------------|-----------|
| 1. | Sirahisi wa Zanzibar tunasema | si rahisi |
| | Balahau Kupata urahisi | Si rahisi |

2. Mtu akiwa mlevi hutubia akasamehewa

Tena akiwa msomi msikitini imamu hupewa

Mwafulani kitendo unotenda Uimamu hauwezekani

3. Baba Amani tutajibu kina mama

Uyo kiongozi wao Na bi Kipini kafanana

Sidiria hafu twaazimana japo kuwa langu pana

Baba Amani usijibu tutajibu kina mama

Asojua aibu si mtu huyo ni nyama

12. TANZANIA

Tanzania muungano nchi mbili

Tanganyika na Zanzibar

Tumesha ungana sie

Twamkumbuka baba Nyerere

Kutuunganisha kuku bali nchi yake

Baba kuibadilisha

Bila wasi wasi babaetu karume

Alikubali muasisi muungano usimame

Tena sote kwa pamoja tulifurahi sana

Muungano ni mmoja sasa tumetulizana

Tuyashike pamoja muungano kutumia.

13. HONGERA HONGERA

Hongera hongera wee sote tumpongezeni

Hongera hongera wee sote tumpongezeni

Kiongozi wa busara aongoze Tanzani

Baba Mkapa hongera

kamata vyema sukani.

Hongera hongera weeSote tumchagueni

Hongera hongera weeSote tumchagueni

Kiongozi wa busara

Kwetu hana mpinzani

Baba Mkapa hongera

Ondoa shaka kichwani.

Hongera hongera weeTusifanyeni utani

Hongera hongera weeTusifanyeni utani

Kiongozi wabusara

Tunae huyu jamani

Baba Mkapa hongera

Sote tunakuamini.

Bankapa mkweli we kamjalia muumba

Zitizameni dalili mwenza kamtoa Pemba

Mkapa mtu mkweli kwa kura tutampamba

14. KOMANDO SALMINI

1. Ndugu wapinzani wanasema turudi ya Zamani

Mji mwisho mikunguni na kangili ziwe Pemba mjini hizo

CCM we imeshika usukani inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini

2. Mapinduzi mwayalani sera zenu kutoka Arabuni

Miti yote iko chini mmejenga mpaka Magogoni

CCM we imeshika usukani inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini

3. Kinamama mfikiri cha CUF sio chama chenu

CCM ni hodari yasomesha hao watoto wenu

CCM we imeshika usukani inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini

4. CUF imevaa tai kiunoni wamefunga herizi

Nyumba waloweka tawi ni faida ya Mapinduzi

CCM we imeshika usukani inazidi kwenda mbele na nahodha Komando
Salmini

5. Komando kaanza kazi kwenye kipindi kigumu

Alofanya yako wazi Tumpongeze kwa mashamsham

CCM we imeshika usukani inazidi kwenda mbele na nahodha Komando

Salmini

6. Mapinduzi mwa yalani sera zenu za kishetani

Maendeleo hamuoni mmeganda nyumba za Michenzani

CCM we imeshika usukani inazidi kwenda mbele na nahodha Komando Salmini

Komando ndo dereva uyoo Tumempenda wenyewe

Wabayacheke naoo Tumempenda wenyewe

CUF awapa chajio hao Tumempenda wenyewe

Chanzo : bi Fatma Ali Khamis wa kikundi cha imarisha

Hizi ni nyimbo zilizoimbwa na kikundi cha East Africa Melody

15. WASO HAYA WANAMJI WAO

Waso haya wana mji wao

Binaadamu waso haya wana mji wao

Hawana lililo baya kwa upande wao

Jambo wakikutendea nisawa sawa kwao

Waallahi masikini roho zao

Wazuri sura jamali maumbile yao

Kumbe ni watu thakili tabia zao

Huchunga na kusaili mambo ya wenzao

Yao huyaficha mbali vibindoni mwao

Kweli wasohaya wanamji wao

Warambaji visogoni watu wa namna hao

Majungu na kufitini ndio kazi yao

Tonge yako kwenda kinywani hawapendi wao

Hata ukiwathamini huna jema kwao

Wasohaya hawajali utu wao

Wasohaya wanafanana hata sura zao

Kupuliza na kutafuna ndio kazi zao

Nyuso wameshazichuna kwa umbea wao

Wenyewe wanajuana wana mji wao

Naona yatawashinda ni hasara kwao

Kiitikio

Wasohaya wana mji wao

Wasohaya huna jema kwao

Wasohaya hawaoni yao

Waallah masikini roho zao

16. NJANGU HATA WEWE

Ewe njangu ewe, ewe hata nawe

Oh! Unanichekesha basi hata nawe

Hadhi yako imekwisha, wacha nijifaraguwe

Hivyo leo nakupasha, njangu usijizuzuwe

Oh! Kwangu hutotamba, leo sio jana

Hata ukiniperemba, mimi kwake nishabana

Tunalisakata rumba, maraha tuna peyana

Bure unavyojigamba, njangu hutakiwi tena

Oh! Njangu masikini, iwe hata nawe

Hebu jiweke pembeni, tayari nipo mwenyewe

Nina kolofikisheni, nitashindwaje na wewe

Kabisa hatulingani, njangu mimi sio wewe

Ewe kwake huna soko, wajifedhehesha

Mimi ni kiboko yako, unanitambua tosha

Tamba kwenye matambiko, amini hutonitisha

Kufanana nawe mwiko, njanguunanichekesha

Kiitikio

Unanichekesha, unanichekesha!

Mimi sio wewe, mimi unituwe

17. FISADI KIWEMBE

Jamani mnamjuwa huyo fisadi kiwembe au mnamsikia tu

Naam tunamjuwa huyo fisadi kiwembe mgombanishaji watu

Mgombanishi femili, mfitini majirani msambaratisha pembe

Yumo miongoni mwetu roho yake ina kutu

Tatizo lake hapendi maendeleo ya mtu

Fisadi kiwembe ana roho mbaya

Ewe fisadi kiwembe hebu acha laana zako

Kazi unayoijuwa kugombanisha wenzako

Bibi wewe ni mbeya uongo ndio sera zako

Kila nyumba waingia kuanzisha chokochoko

Pia unakuwadia mabwana wa shoga zako

Na kuvunja zao ndoa kwa choyo na wivu wako

Watu wameshaamuwa unatafutwa mnoko

Kosovo utashushiwa ukome umbeya wako

Unajaza Masusu kwa mambo yasokuhusu

Kwenye harusi hutoki kwa kutafuta undanu

Matangani huanduki ujuwe kalala nani

Kwa majungu hushikiki wenziwe kuwafitini

Siri za watu huchoki kuzimwaga hadharani

Pia umegunduliwa kuwa wewe shuga mami

Dogo dogo wachukuwa kuwafundisha uhuni

Huna hata kuchagua Mungu ameshakulani

Bibi wewe nifasiki choyo choyo kimeshakusibu

Mwenye husuda na chuki maovu umesharabu

Mtu akipata dhiki unafurahi ajabu

Senti akiimiliki una mroga kwa babu

Kuposwa mtu hutaki uchumba unaharibu

Mtu akila vizuri unavimba kwa ghadhabu

Akipendeza kwa nguo bibi roho yakuuma

Kitembea kwa matao matumbo yakunguruma

Fisadi usojjuwa ukome umbeya wako

Kitikio

Ewe fisadi kiwembe hasidi roho za watu

Umestadi umbeya mgombanishaji watu

Tatizo lake hapendi maendeleo ya watu

Pia unashutumiwa kwa kuwachanisha watu

Kiumbe ulolaaniwa roho yake ina kutu

Watu wanakutafuta kwa uvumba na udi

Hadharani kukusuta ukomeshwe ukuwadi

Bibie utaipata ujute kuwa fisadi

18. KINYANGUNYA

Kiitikio

Kinyangunya usitaake ya watu kinyangunya

Kinyangunya yako yanakushinda kinyangunya

Kinyangunya usitake ya watu kinyangunya

Kinyangunya yako yanakushinda

Kinyangunya kumbe hujagoya ila si bure umerongwa

Kinyangunya kumbe hujagoya si bure we umerogwa

Nasikia wewe nasiki wewe unajitapa

Nasikia wewe nasikia wewe unajitapa

Watu ukiwajulisha wewe ukiwajulisha

Watu ukiwajulisha wewe ukiwajulisha

Eti ninakuogopa ninakuogopa wataka kunionesha

Kitu gani wajitapa una nini kibahasha

Kanzu yako ya rubamba utaye mliza nani

Ina vipande vipande karibu ya thalathini

Kanzu yako ya rubamba utayemliza nani

Ina vipande vipande karibu ya thalathini

Abebeduwa wenziwe yeye

Yeye ajione kwini

Apiga watu vikumbo

Tumjuwe yeye nani

Vicheko vinagongana he he he

Wengine wanafinyana naye huyu huyu kafata nini

Isha wanaulizana naye huyu kaja saa ngapi

Kinyangunya hupendezi hata ukivaa nini

Kinyanyungunya hupendezi hata ujipambe vipi

Ya mjini huyawezi kinyangunya

Yangoje ya kijijini

Watamba eti nawe watamba eti ndio mwenyewe

Wamba eti nawe watamba et indo mwenyewe

Kila kitu wamechisha eti nawe wamechisha

Kila kitu wamechisha eti nawe wamechisha

Na uliye naye wewe naye wewe mambo unamridhisha

Nambiye ndiye wewe shoga mbona umechusha

Umenyorodoka wewe karagosi unatisha

Umenyorodoka wewe karagosi unatisha

Usoi umejipamba kwa mashedo unatisha

Uwanjani unatamba viroja unaonesha

Usoni yeye usoni

Usoni amejipamba kwa mashedo anatisha

Uwanjani anatamba viroja anaonesha

Hatutakwenda sambamba mwenzangu unachekesha

Hatutokwenda sambamba mwenzangu umechemsha

Kinyangunya vipodozi hujwi upake nini

Mchana wa jua kali mingaro iko machoni

Usiku ukiingia unajifanya umewini

Chanzo : Hidaya Khamis wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar

Hizi ni nyimbozilizoimbwa na kikundi cha uhamasishaji cha Chama Cha Wananchi

(C U F)

19. CHEREEKO CHEREKO

Chereko chereko C.U.F tuko furahani

Chereko chereko C.U.F tuko furahani

Ikulu tutaingia kwa salama naamani

Ikulu tutaingia kwa salama naamani

CCM tawang'oa tutawashinda yakini

Tutakuzisha amani raha tupu Visiwani

Musiwe na wasiwasi CUF mwaka huu mwaka wetu

Tutatawala wenyetu Ikulu takuwa yetu

Siku tunaisubiri Sefu kwenda uwanjani

Kukabidhiwa sukani Sefu hana mpinzani

Wana CUF chereko chereko aeeee Chereko chereko

Kina mama chereko chereko aeeee Chereko chereko

Na vijana chereko chereko aeeee Chereko chereko

Na ikuli chereko chereko aeeee Chereko chereko

Mwaka huu chereko chereko aeeee Chereko chereko

20. CHAGUO LETU NI WEWE MAALIM SEIF SHARIF

Kura zote kwako wewe dunia yote ikusifu

Kwanza twakupa pongezi Rais wetu mtarajiwa

Seif Sharif mchapaka kazi vizuri tunakuelewa

Milango yote iko wazi ikulu tushaifungua

Kwakujua wazi wazi maendeleo utatuletea

Tutakupa kura zote kushinda kwako lazima

Tuna hakika kwa wote utauongoza umma

Na kwa kishindo upite tuyasahau ya nyuma

Maendeleo ulete tusirudi tena nyuma

Kiitikio

Kura zote tunakupa wewe C.U.F hatufanyi ajizi

Na wewe ndie mwenyewe ndie wetu mtetezi.

21. HELUWA

Heluwa heluwa heluwa C.U.F yetu

Heluwa heluwa heluwa Zanzibar yetu

Heluwa heluwa, heluwa Seif wetu

Kwa itikadi ya chama na ilani tuloweka

Seif tumesha muona na ndomana tukampa

Kaahidi wazi wazi maendeleo kuleta

Hatofanya upuuzi barazani akifika

Shime na tumchaguwe nchi itabadilika

Si matatizo ya maji na mengine ya kwisha

Haya haya wa bububu mwananyanya kijichi ndani

Na mlo mjimkongwe nyote tumpelekeni

Kwa kura yetu ya C.U.F Nchi iwe mikonononi

Hakika huyu tabibu, wa maradhi visiwani

Kiitikio

Heluwa heluwa heluwa heluwa

Heluwa Seifu heluwa

Ndio mkombozi wetu ang' arishe nchi yetu

Chanzo Hisham Khamis Haji wa Chama Cha Wananchi

Hizi ni nyimbo zilizoimbwa na kikundi cha Tanzania One Theater

22. PISHA NJIA

Pisha njia eee pisha njia eee

Hao wanakuja, hao wanakuja CCM

Pisha njia ee pisha njia hao wanakuja CCM

Tupishe tupishe wee hao wanakuja CCM

Gari kubwa hilo linapita

Watanzania panda gari kubwa CCM

Wapinzani panda gari kubwa hilo

Gari kubwa hilo linapita

Pisha njia wee pisha njia hao wanapita CCM

Gari kubwa wee pisha njia hao wanapita CCM

Wpinzani ee ingieni hao wanapita CCM

Watanzania CCM ya wina

Watanzania CCM ya wina

Vijana CCM ya wina

Vijana CCM ya wina

Kina mama CCM ya wina

Kina mama CCM ya wina

Walimu CCM ya wina

Wanafunzi CCM ya wina

Mama lishe CCM ya wina

Baba lishe CCM ya wina

Madereva CCM ya wina

Wapiga debe CCM ya wina

23. HARAMBEE

Harambee harambe baba harambee

Harambe harambe mama harambee

Wapinzani tuwalete tuwachanachane tuwatupe

Makafu tuwalete tuwachanechane tuwatupe

CCM tuwalete tuwakumbatie tuwabusu

Amani tumlete tumkumbatie tumbusu

Seifu tumlete tumchane chane tumchome

Lipumba tumlete tumchanechane tumchome

Harambee harambe baba harambee

Harambe harambe mama harambee

Chanzo :Mwanaidi Harouob mpenzi wa Chama Cha Mapinduzi

Kiambatanishi 2: Hojaji kwa Walimu na Wasomi

Ndugu mpendwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu

Zanzibar kuanzia 2000 hadi 2010. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu kwa jamii ya Wazanzibari, hatimae kudhihirisha na kuwasilisha matokeo yenye suluhu ya kuleta amani, usawa na umoja miongoni mwa wanajamii.

Ninakuomba sana, na nitakushukuru sana kama utayajibu maswali ya dodoso hili.

Utakuwa ni mmoja wa wazanzibari wenye kupenda umoja na uzalendo. Mchango wako huu utathaminiwa sana.

Mtafiti anakuomba usiwe na hofu wala wasiwasi katika kujaza kwako dodoso hili.

Majibu yote utakayoyatoa yatahifadhiwa, na kutunzwa na hayataolewa. Kwa mnasaba huu usiandike jina lako sehemu yoyote katika dodoso hili.

Sehemu ya kwanza

Taarifa binafsi za mtafitiwa

Umri wako

Jinsi

Kazi yako

Kiwango chako cha elimu

Mahali unapoishi

Sehe mu ya pili

Taarifa kuhusu utafiti

1. Umewahi kusikia nyimbo za kampeni ya uchaguzi ndio _____ hapana.

2. Nyimbo hizo umezisikia wapi?

a) Viwanjani (b) Redioni (c) Mitaani

3. Unapenda kusikiliza nyimbo hizo

Ndiyo _____ hapana _____

4. Wewe ni (a) msanii, (b) Msikilizaji (c) Mpenzi

5. Kama ni msanii umewahi kutunga au kuimba nyimbo za kampeni ya uchaguzi:

Ndiyo _____ hapana _____

6. Kama jibu ndiyo, taja nyimbo tatu (3) ulizowahi kutunga au kuimba

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

c. Kama ni mpenzi taja nyimbo tatu (3) unazopenda zaidi

- (i) _____
- (ii) _____
- (iv) _____

d. Kwa nini ulizichagua nyimbo hizo. Toa maelezo machache.

7. Eleza kwa ufupi kwanini unapenda au unatunga au unaimba nyimbo za Kampeni ya uchaguzi.

8. Nyimbo za Kampeni ya uchaguzi ni sehemu ya fasihi, kama fasihi nyengine, huwa na mambo maalum yanayofanikisha kazi hiyo. Taja mambo mawili (2)

- (i) _____
- (ii) _____

9. Unafikiri nyimbo za Kampeni za Uchafuzi Mkuu wa Zanzibar zina madhumuni maalum. Ndiyo _____ Hapana _____ Sijuwi _____

10. Kama unakubali kuwa nyimbo za kampeni zina madhumuni maalumu, taja madhumuni matatu (3).

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

11. Watu wa Zanzibar wanazipenda nyimbo za kampeni ya uchaguzi kwa sababu ya

(a) Lugha inayotumika

(b) Mitindo inayotumiwa katika kuimba

(c) Madhumuni yaliyomo katika nyimbo hizo

12. Nyimbo za kampeni za uchaguzi zinaelimisha jamii.

(i) Sana _____ Kidogo _____ Kidogo sana
_____ hazielimishi.

13. Nyimbo hizo zinajenga au zina vunja umoja wa Wazanzibari.

14. Je Nyimbo za kampeni za uchaguzi zinamchango gani kisiasa na kiutamaduni kwa Wazanzibari?

15 Toa maoni yako kwa jumla kuhusu Maudhui ya nyimbo za Kampeni ya uchaguzi Mkuu wa Zanzibar.

**Kiambatanishi 3: Muongozo wa Mahojiano na Wadau Mbalimbali wa Nyimbo
za Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar Wakiwemo Wasanii,
Vijana, Walimu, Wataalamu wa Lugha ya Kiswahili, Wasomi na
Waandishi wa Habari**

Ndugu mpendwa,

Ninafanya utafiti kuhusu Maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu

Zanzibar kuanzia 2000 hadi 2010. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza maudhui ya nyimbo za kampeni za uchaguzi mkuu kwa jamii ya Wazanzibari, hatimae kudhihirisha na kuwasilisha matokeo yenye suluhu ya kuleta amani, usawa na umoja miongoni mwa wanajamii.

A: Taarifa Binafsi za Muhojiwa

1. Jina la muhojiwa
2. Pahala yalipofanyika
mahojiano.....
3. Hadhi /cheo cha muhojiwa
4. JinsiaUmri.....
5. Tarehe na muda wa mahojiano.....
6. NO Simu Anuani ya Posta

B: Maswali ya Mada ya Utafiti

7. Kwa mawazo yako unafahamu nini kuhusu nyimbo za kampeni?
8. Nini faida ya nyimbo za kampeni ya uchaguzi
9. Nini hasara ya nyimbo hizo

10. Wewe umewahi kushiriki katika kuimba, kutunga au kusikiliza nyimbo za Kampeni?
11. Je, kuna tofauti gani ya nyimbo za kawaida na nyimbo za kampeni za uchaguzi.
12. Kama zipo taja tofauti tatu (3)
13. Je unahisi nyimbo za kampeni zinawagusa vipi watu?
14. Je, nyimbo za kampeni za uchaguzi zina usanii gani ndani yake au zinafurahisha tu?
15. Maudhui ya nyimbo hizi watu huyatumia vipi?

Toa maoni yako kuhusu nyimbo za kampeni za uchaguzi.